ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Pili - Tarehe 24 Novemba, 2016

(Kikao kilianza Saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Zuberi Ali Maulid) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 145

Utekelezaji wa Ahadi ya Ujenzi wa Barabara ya Fuoni Kitongani

Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Aliuliza:-

Kwa kuwa mnamo mwaka 2008 aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, alitembelea Skuli ya Fuoni Kitongani na aliahidi kutengeneza barabara kutoka Fuoni Meli Sita kuelekea Skuli ya Fuoni Kitongani.

(a) Je, Wizara yako iliwahi kufuatilia utekelezaji wa ahadi hii.

(b) Je, azma ya kujengwa barabara hii kama ilivyotolewa ahadi na Rais bado ipo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 145 lenye kifungu (a) na (b) naomba kutoa maelezo kama ifuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, nakubali kwamba mnamo mwaka 2008, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya M. Kikwete, alitembelea Skuli ya Fuoni Kitongani na aliahidi kuitengeneza barabara kutoka Fuoni Meli sita hadi Skuli ya Fuoni Kitongani. Kufuatia ahadi hiyo, mnamo tarehe 09-12/02/2016 Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Muungano na Mazingira ilifanya ziara iliyoongozwa na Naibu Waziri wa Wizara hiyo Mhe. Luhaga J. Mpina ya kutembelea barabara hiyo na maeneo mengine, ambayo Mhe. Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne (4) wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliahidi kuyaboresha.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba nimjibu Mhe. Mjumbe, swali lake nambari 145 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, wizara yangu tayari imeshafuatilia ahadi hii na kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Usafirishaji tayari imepokea makisio ya gharama stahiki na tayari makisio hayo yameshawasilishwa katika Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa hatua zaidi.

(b) Mhe. Naibu Spika, azma ya kujengwa barabara hii bado ipo na utekelezaji wake utaanza mara tu fedha hizo zitakapopatikana. Ahsante sana.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze tu Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake aliyoyaeleza na ya ufasaha kabisa. Mhe. Naibu Spika, nataka niulize swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri, kama alivyosema kwamba tayari wameshafanya makisio na wameshapeleka kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais na Mazingira ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Je, ni lini barabara hiyo itatengenezwa baada ya kupelekwa makisio hayo?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi kwamba dhamira ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na dhamira ya Serikali ya Zanzibar ni kuhakikisha utekelezaji wa barabara hii, ama ujenzi unakamilika. Hivyo, wizara yangu tayari imeshafanya mawasiliano ya kina, na hata juzi tu bahati nzuri sana Mhe. Naibu Spika, mimi mwenyewe binafsi kwa kushirikiana na watendaji na kwa kushirikiana na viongozi, Masheha na Madiwani husika kutokea mwanzo wa barabara ile tumeshaikagua na sote tumeshalithibitisha hilo.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, tunamuomba Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni atustahamilie, utaratibu wa kiutendaji unafuatwa na utakapokamilika ujenzi rasmi utaanza katika barabara hii. Ahsante.

Nam. 122

Uwekaji wa Sare kwa Watumishi wa Serikali

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafanya shughuli zake kwa kupitia Wizara na Idara zake kwa ufanisi na kwa kutekeleza malengo ya maendeleo kwa wananchi wake kwa ufanisi zaidi. Lakini kupitia Wizara na Idara hizo wafanyakazi wake hawana nguo na sare za kazi zao kama ilivyo katika sekta nyengine za kibenki, majeshi, polisi na nyenginezo.

(a) Je, Serikali ina sare maalum kwa wafanyakazi wa wizara zake zilizowekwa kisheria.

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kueka sare za wizara au idara ili kuondoa usumbufu kwa wananchi kutokuwatambua wafanyakazi hao pamoja na kupunguza utoro kwa wafanyakazi.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka taratibu za kinidhamu kwa wafanyakazi wanaokiuka utaratibu huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 122 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi, naomba kutoa maelezo yafuatayo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba, ni kweli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafanya shughuli zake kupitia wizara na idara zake, kwa ufanisi na kwa kutekeleza malengo ya maendeleo kwa ajili ya wananchi wake. Aidha, ni kweli kwamba watumishi wa wizara na idara hizo hawana sare maalum kama ilivyo kwa sekta nyengine kama majeshi, polisi na benki.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

a. Mhe. Naibu Spika, Serikali haina sare maalum kwa watumishi wanaofanya kazi katika wizara zake. Hoja hii imefafanuliwa vizuri kwenye Kanuni ya 34 (1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014, ambazo hazijaweka sare maalum kwa wafanyakazi hao, badala yake zinamtaka mtumishi wa Umma kuvaa kivazi kilichosafi chenye kuhifadhi heshima yake na kinachokubalika katika maadili na utamaduni wa Kizanzibari.

b. Mhe. Naibu Spika, pamoja na uzuri na umuhimu unaojitokeza kwa watumishi wa wizara na idara kuvaa sare, lakini kutokana na bajeti serikali isingeweza kuwapatia sare watumishi wote. Hali hii inatokana na matakwa ya kisheria kama inavyofafanuliwa katika kanuni ya 34 (2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma kwamba;

"Iwapo mtumishi wa umma atahitajika kuvaa sare katika sehemu yake ya kazi, sare hiyo itatolewa kwa gharama za serikali".

Mhe.Naibu Spika, pamoja na maelezo hayo, napenda kutumia fursa hii kumthibitishia Mhe. Mwakilishi kwamba hakuna usumbufu ulioripotiwa kujitokeza kutokana na wananchi kutowatambua watumishi kwa sababu za kutokuvaa sare. Aidha, napenda kumthibitishia Mhe. Mwakilishi kwamba, tabia ya utoro kazini kwa Watumishi wa Umma haitokani na kutokuvaa sare bali inatokana na mambo mengine binafsi, ikiwa ni pamoja na khulka ya Mtumishi mwenyewe.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo, serikali haikuzuia watumishi wenyewe binafsi au Taasisi za Umma kuwaruhusu watumishi wake kuvaa sare, iwapo watumishi husika au taasisi hizo zina uwezo wa kugharamia sare hizo. Kinachosisitizwa ni kwa mtumishi kuvaa kivazi kilichosafi, chenye kuhifadhi heshima yake na kinachokubalika katika maadili na utamaduni wa Kizanzibari.

c) Mhe. Naibu Spika, serikali tayari imeshaweka taratibu za kinidhamu kwa watumishi ambao huvunja maadili ya Utumishi wa Umma wakiwemo watumishi wanaotoroka kazini. Kwa kawaida, hatua za kinidhamu huchukuliwa kwa mtumishi huyo kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma nambari 2 ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2014.

Mhe.Naibu Spika, kwa kuwa hivi sasa serikali haijaweka utaratibu wa kuvaa sare kwa watumishi wake wa mawizara na idara, hivyo, hata taratibu za kinidhamu juu ya ukiukwaji wa utaratibu huo haujawekwa katika Kanuni na

Miongozo yetu ya Utumishi wa Umma. Iwapo serikali itaamua kuanzisha utaratibu wa watumishi wake kuvaa sare, basi taratibu za kinidhamu pia zitawekwa ili kuona kwamba, mtumishi atakaekiuka utaratibu huo anachukuliwa hatua kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru sana Mhe. Naibu Spika, na namshukuru Mhe. Naibu Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ameelezea vizuri sana. Mhe.Naibu Spika, pamoja na maelekezo aliyotoa, bado nasema kwamba kumejitokeza utapeli mwingi sana na mambo mengi sana kutokana na vitambulisho vya sare na mambo mengine.

Naomba kumuuliza swali la nyongeza kwamba kama sare bado labda serikali haina uwezo wa kuzipata,

(a) Je, hata vitambulisho ambavyo vina picha ya mtu anapofanyakazi yake. Hata hivyo, serikali imeshindwa kuwapatia. Hilo ni swali (a).

(b) Hawaoni kwamba kuwavalisha sare katika wizara au idara pia ni unadhifu fulani wa kutokuoneshana mavazi au baadhi ya nguo kwa wafanyakazi au kwa kushindana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, haijashindwa kutoa vitambulisho kwa wafanyakazi wake.

(a) Mhe. Naibu Spika, ukweli ulivyo baadhi ya wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi wa Zanzibar, vitambulisho wanavyo na kama wapo basi ni wachache tu ambao hawana. Hata hivyo, nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake kwamba, hawa wafanyakazi ambao vitambulisho mpaka dakika hii hawajapata, basi wakati wote kutoka sasa hivi tunaweza kuwapati vitambulisho hivyo.

(b) Mhe. Naibu Spika, kutokuwepo kwa sare kwa wafanyakazi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hakutoleta ubaguzi. Lakini wazo lako ni zuri kama ambavyo umeuliza swali lako la msingi, kuwa ni vyema wafanyakazi wetu wakawa na sare. Kwa hivyo, wazo lako tumelichukua na tutalifanyia kazi ipasavyo ili kuhakikisha kwamba wakati utakaporuhusu wafanyakazi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanakuwa na sare, ili waweze kupendeza na popote pale mtu atakapokuja ajuwe kwamba huyu ndiye mfanyakazi wa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Mimi naitwa Suleiman Makame Ali. Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, baadhi ya wafanyakazi wa taasisi za serikali hufanyakazi kwa mazowea, wakiwemo hao watoro wa makazini.

Je, ni hatua gani zinazochukuliwa kwa wafanyakazi hawa wazembe.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kabisa baadhi ya wafanyakazi huwa wanafanyakazi kwa mazowea. Lakini naomba Mhe. Naibu Spika, ikumbukwe kwamba suala la kufanyakazi kwa mazowea, huwa linakemewa pamoja na viongozi wengine na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi huwa analikemea sana suala hili, na hata katika hotuba yake ya ufunguzi, alilizungumza hili katika Baraza letu kwamba tusifanyekazi kwa mazowea.

Kwa hivyo, wale wote ambao huwa wanafanyakazi kwa mazowea hatua zimeshaanza kuchukuliwa na zitaendelea kuchukuliwa na zitachukuliwa zaidi, ili kuhakikisha kwamba wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufanyakazi kwa mazowea kuwe kuna mwisho wake.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Waziri, naomba tupatiwe idadi ya wafanyakazi waliochukuliwa hatua kwa makosa ya kinidhamu katika mawizara.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, swali lake nimelipokea, nimelichukua na nina ahidi nitakuletea kwa maandishi, ili kukupa hiyo orodha ya hao wafanyakazi waliochukuliwa hatua kwa ajili ya kufanyakazi kwa mazowea. *(Makofi)*

Nam. 15

Tatizo la Uchakavu wa Nyumba za Askari Magereza

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Nyumba za askari wa Magereza zinakabiliwa na uchakavu mkubwa na kusababisha faragha zao kuvunjwa kutokana na familia moja kuishi chumba kimoja na kushindwa kutembelewa na wazazi wao na jamaa zao wakati ni

kinyume na kifungu cha 13 Mabano (1) cha Katiba ya Zanzibar juu ya Haki ya kuwa na Hifadhi.

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani ya kuondoa tatizo la uchakavu wa nyumba za Magereza Unguja na Pemba pamoja na kuweka familia moja chumba kimoja wakati ni kinyume na msingi wa Haki za Binaadamu.

(b) Je, Kwa nini katika Chuo cha Mafunzo, Serikali imeshindwa kutumia wanafunzi wake kusaidia kuondoa tatizo la makaazi kwa kujenga nyumba za kuishi askari kwa kutumia ujuzi waliokuwa nao na nguvu kazi badala ya kutegemea Serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 15 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa baadhi ya nyumba za Maofisa, na Askari wa Chuo cha Mafunzo ni chakavu. Aidha, zipo nyumba za chumba kimoja ambazo zimekusudiwa kwa askari ambao hawajawa na familia. Hata hivyo, nyumba hizo za chumba kimoja zimekuwa zikikaliwa na askari wenye familia kinyume na makusudio kutokana na uhaba wa nyumba uliopo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kutambua hali hiyo isiyoridhisha kwa askari wetu, Chuo cha Mafunzo kina mpango wa kujenga nyumba kwa askari wenye familia katika magereza yake ambazo zitazingatia faragha ya wakaazi wake. Aidha, kazi ya kuzifanyia matengenezo nyumba kongwe zilizopo inaendelea.

(b) Mhe. Naibu Spika, Chuo cha Mafunzo kinatumia askari na wanafunzi wake katika kazi mbali mbali zikiwemo za ujenzi. Kwa kufanya hivyo sio tu chuo kinatekeleza miradi yake ya ujenzi, bali pia kinatoa fursa kwa wanafunzi kujifunza na kupata ujuzi ambao wanatarajiwa kuutumia baada ya kukamilisha kutumikia adhabu zao chuoni hapo. Hata hivyo, miradi ya ujenzi hasa wa nyumba za makaazi ya askari,

unatekelezwa kulingana na upatikanaji wa vifaa vya ujenzi, kama vile saruji, nondo, mabati, mbao, n.k. Hata hivyo, mara kadhaa upatikanaji wa vifaa hivyo huathiriwa na ufinyu wa bajeti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Jana Mhe. Naibu Waziri, nilimuuliza masuala mawili lakini akanijibu moja, lakini nikajua ni mgeni bado na mimi nikastahamili, mtoto akizaliwa hutambaa, hukweta akapata mguu akaanguka baadae, lakini leo naomba anisikilize kwa makini kabisa, ndio anakuwa hivyo.

Tatizo hili ni la muda mrefu na Serikali itachukua kipindi gani kuliondoa tatizo hili juu ya askari wetu hao kwa sababu haki ya faragha ni jambo la msingi na wanaendelea kuteseka, na majibu ya Serikali, Serikali imo mbioni muda mfupi tu, tutajipanga na ujenzi huo. Hilo la kwanza.

La pili, katika majumba yaliyojengwa *block No.* 9 na 10 zilizojengwa na Serikali, kuna sababu gani za msingi kunyimwa askari wale wa magereza na badala yake, sitaki kusema kuna viongozi wanamiliki zaidi ya nyumba mbili, na wengine kumiliki nyumba katika maeneo yale.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Muwakilishi swali la nyongeza la (b) alirejee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, ikiwa la mwanzo ameshalipokea na la (b) si tatizo. Katika nyumba zilizojengwa hivi juzi *block No.* 9 na 10 kuna sababu gani za msingi askari wale ambao ndio tegemeo letu wasipewe nyumba zile kuishi, na badala yake kuna viongozi wanamiliki zaidi ya moja mle ndani.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Sika, ni kweli amesema kwamba inakuwa ni kawaida kila siku majibu yanatoka kwamba labda ni baadae, lakini naomba Mhe. Mwakilishi arejee suala langu la awali au la msingi ambalo nimemjibu kwamba hali hii si kwamba Serikali inaridhika na mwenendo huo au hali hiyo iliyopo.

Na badala yake ni kwamba imetokana na sababu maalum ambazo zinatokana na masuala mazima ya upatikanaji wa fedha ambapo jambo hili nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi, kwamba pale ambapo hali ya fedha itaruhusu namhakikishia kwamba kama tulivyosema kwamba kazi hiyo tayari imeshaanza kuendelea nadhani changamoto hiyo tunaahidi kwamba itaweza kutatuka, tunachoomba ni fedha tu ndio changamoto ambayo tunaweza kuipata.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, tusubiri Mhe. Waziri, amesimama tuendelee haya.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, jibu (b) napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba bado naendelea kusema kwamba kama tulivyotanguliza kutoa majibu, kwamba suala ambalo amesema kwamba hili limetokana na uchache wa fedha na uhaba wa nyumba tulionao, lakini pamona na suala alilouliza nimwambie kwamba taarifa hiyo bado haipo vizuri na hiyo taarifa ambayo imetolewa nadhani kwamba tutaichukua na kuifanyia kazi tuone kama jambo hili lipi basi tuone kwamba tunakaa na kuweza kulitatua.

Lakini bado tukumbuke kwamba changamoto tuliyonayo itaendelea kuwepo na itaondoka pale ambapo fedha zinaweza kupatikana kwa wakati na mahitaji ambayo tunazihitaji. *(Makofi)*

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

Mhe. Naibu Spika: Kuhusu utaratibu Mhe. Jaku.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na ugeni wake narudia tena Mhe. Naibu Waziri, nilichokizungumza ni kidogo sana na kifupi, nafikiri Kanuni ya (37) inaturuhusu suala kujibiwa na Waziri mwengine au Mwanasheria Mkuu, nafikiri Waziri atatusaidia bosi wake.

Katika nyumba *block No.* 9 na 10 zilizojengwa na Serikali kuna sababu gani ya msingi kutokunyimwa askari askari wale wa magereza na wengine wakiwa wameshiriki katika kujenga nyumba hizo, na baadae viongozi wakamiliki maeneo yale.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa majibu ya ziada

juu ya masuali ambayo yameulizwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub na kujibiwa na Mhe. Naibu Waziri Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Naibu Spika, katika suala lake Mhe. Jaku, amekoti kifungu cha Katiba Nam. 13, chenye maneno ya pembeni, yaani *marginal note,* haki ya kuwa hai, kifungu hicho cha 13(1), kinasema;

"Kila mtu anayo haki ya kuwa hai na hifadhi ya maisha yake".

Kifungu cha 13(2), kinasema;

"Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake kwa mujibu wa sheria".

Kifungu 23(3), kinasema;

"Ni marufuku kwa mtu kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazowezwa au kumdhalilisha mtu".

Mhe. Naibu Spika, kifungu hiki kinahusu hifadhi na kama nilivyokinukuu, ni vizuri Mhe. Jaku, aelewe anapotumia vifungu vya Katiba atumie kwa maana iliyokusudiwa na tafsiri yake.*(Makofi)*

Chuo cha Mafunzo kupitia Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa G1na Idara Maluum za SMZ, hakijawahi, hakitawahi, wala hakitamtesa na kumkosesha uhai askari yeyote ambaye amejiunga na Chuo cha Mafunzo, kama alivyoeleza Mhe. Naibu Waziri, na nataka nichukue fursa hii kumpongeza sana kwa majibu yake mazuri ambayo ameyatoa ya kueleza kwa nini askari wetu wanaendelea kukaa kwenye nyumba chakavu, na juhudi za Serikali kupitia Chuo cha Mafunzo zinazochukuliwa kwa kuondosha tatizo hilo.

Lakini la pili aelewe kwamba nyumba za familia moja au za chumba kimoja wanakaa askari *single,* yaani ambao hawajaoa wala hawajaolewa, tatizo liliopo kwamba askari ambae hajaoa au hajaolewa anapopewa kukaa kwenye chumba cha kukaa *single,* anapoowa kutokana na hali yake ya maisha anakuwa hataki kuhama kwenye nyumba ile, na sisi kama Serikali au kama Chuo cha Mafunzo hatuwezi kumlazimisha kwa sababu yule ni mtumishi wa Chuo cha Mafunzo.

Kwa hivyo, Mhe. Jaku, atustahamilie kwamba kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri, kwamba Serikali kupitia Chuo cha Mafunzo itaendelea kujenga

nyumba za askari, na pale hali itakaporuhusu basi askari wetu watakaa kwa nafasi na kwa mujibu wa hali itakayokuwepo.

Ni kwa nini Serikali imezigawa nyumba za Michenzani na isiwape askari, tokea mwanzo nyumba zile zilijengwa kwa dhamira ya kuwapa wananchi, *block No.* 10 ni *block* ambalo wamepewa wananchi hasa wale ambao walivunjiwa nyumba zao na walikuwa bado hawajapewa nyumba za Serikali zilipotolewa zile nyumba za Michenzani. Nyumba zilizobakia zimekodishwa kwa wananchi wa Zanzibar; awe kiongozi, awe mkurugenzi au awe raia huyo ni mwananchi na ndio lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Machano Othman Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuuliza suala langu, kwanza napenda nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri, na Mhe. Waziri, kwa majibu yao. Suala langu la nyongeza ni kama ifuatavyo.

Kwa kuwa tatizo la makaazi kwa askari wetu wa SMZ, sio kwa Chuo cha Mafunzo tu, ni kwa vikosi vyote vitano, na kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri, tulitembea pamoja na aliona tatizo hili lilivyo na zaidi Pemba kama Tungamaa na sehemu nyenginezo.

Je, Serikali haioni kwamba wakati umefika sasa kwa vile bajeti ya Wizara hii peke yake haiwezi ikamaliza tatizo la nyumba kwa askari wetu, kuingia makubaliana na mfuko wa *ZSSF* kama ilivyo kwa majeshi yetu ya Jamhuri ambao wamejengewa nyumba na *NSSF*, sisi Zanzibar tutafanya lini ili mpango huu uwezekane na askari wetu waache kukaa uraiani na kukaa katika mahanga hali ambayo inaleta kero kubwa kwa askari wetu.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Kwanza nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi na Baraza lako tukufu kwamba suala la makazi ya askari wote ni *policy* ya Serikali, kwa hivyo, sisi Serikali tutachukua ushauri ambao ameutoa Mhe. Mwakilishi ili tuone katika mipango yetu ijayo ya bajeti ya mwaka ujao wa fedha, kama tunaweza tukakubaliana na wenzetu wa *ZSSF*, ama Serikali ikatafuta njia nyengine kupitia taasisi nyengine za kifedha ili kuona kwamba tatizo hili la ukosefu na uchachewa nyumba za wapiganaji wetu tunalipatia ufumbuzi.

Ni adhima ya Serikali kuhakikisha kwamba jambo hilo tunalipatia ufumbuzi ili askari wetu waweze kukaa katika hali ya maisha mazuri. Ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe.Naibu Spika, kwanza nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Waziri, kwa kujua umuhimu wa maaskari wetu juu ya utumishi wao na kuwa karibu ili kufanya kazi zao vizuri, lakini kwa kuzingatia hali halisi ya nchi yetu hivi sasa hivi askari kukaa pamoja na vyema zaidi kwa usalama wao kuliko kukaa mbali mbali ni hatari kwao.

Je, kwa kuzingatia ardhi yetu sasa hivi ni finyu katika mji wetu huu Mhe. Waziri, ana mpango gani wa kutafuta eneo maalum la vikosi vyetu vya SMZ kujengwa maeneo ya vikosi vya KMKM, Mafunzo, JKU, pamoja na Valantia ili kuwa karibu inapotokea harakati yoyote kupatikana kwa urahisi kwa utendaji wa kazi pamoja na usalama wao wa kuishi, kwa usalama wa kila siku na jamii yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Katika suala lake niseme kwamba adhima ya Serikali kupitia Chuo cha Mafunzo na vikosi vyengine kwa ujumla, ni kwamba tumeshabaini mapungufu au mahitaji ambayo sasa hivi yanahitajika kwa askari wetu na adhima ya Serikali kama nilivyosema mwanzo kwamba ni kuona kwamba mazingira ya vikosi vyetu vinaboreshwa ili kuweza kuona kwamba kazi wanazozifanya zinathaminiwa, na wanaangaliwa zaidi katika kuonekana kwamba wafanye kazi za kisasa na endelevu.

Kwa maana hiyo nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba juhudi kama hizi zinakuwa zinafanyika na sasa hivi kuna baadhi ya maeneo ambayo tayari yanaendeleza ujenzi ambao kwa kweli hapo awali kulikuwa hakuna mpango kama huo.

Kwa hivyo, nimwambie Mhe. Mwakilishi ushauri tunauchukua na tutaufanyia kazi na kwa kadri hali itakavyokuwa imeruhusu kama nilivyotangulia kusema awali, basi nadhani tatizo hili litaondoka ahsante sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Nam. 119

Utaratibu wa Malipo ya Wajumbe wa Bodi Mbali Mbali za Mashirika na Taasisi za Umma

Mhe. Hidaya Ali Makame - Aliuliza:-

Kumekuwa na utaratibu usiowiana wa malipo ya wajumbe kwa Bodi mbali mbali za Mashirika na Taasisi zinazojitegemea za Serikali, ambapo baadhi ya wajumbe wa Bodi hizo hupewa malipo makubwa na wengine malipo yao wastani.

(a) Je, Kuna utaratibu upi au muongozo gani unaotambulika na Serikali wa malipo ya posho za wajumbe wa Bodi.

(b) Kwa nini baadhi ya Bodi zinalipa posho kubwa kwa wajumbe wake.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 119 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

a. Utaratibu uliopo Serikalini kwa malipo ya Wakurugenzi wa Bodi umeainishwa katika Sheria ya Mitaji ya Umma Namba 4. ya mwaka 2002 Kifungu cha 10 kifungu kidogo cha 1 hadi cha 3 inayoeleza kuwa Wajumbe wa Bodi za Mashirika ya Umma watalipwa maposho na malipo ya mwaka baada ya kupendekezwa na Bodi zao na kuidhinishwa na Waziri husika. Utaratibu huu pia unajitokeza katika Sheria zinazoanzisha Mashirika hayo.

b. Kwa hali ya hivi sasa Mhe. Naibu Spika, Kiwango cha malipo ya Wakurugenzi hutegemea uwezo wa kipato cha Shirika/Taasisi husika, mlinganisho wa malipo kwa Taasisi ama hiyo hapa Zanzibar au Tanzania Bara, na haja ya kuwapata Wakurugenzi wenye uwezo na sifa kuitumikia vyema Bodi husika.

Mhe Spika, Pamoja na utaratibu huo unaotumika sasa kama nilivyoueleza, Serikali pia imebaini haja ya kuwa na vigezo maalum vya maslahi ya

Wakurugenzi na wafanyakazi wa Mashirika na Taasisi zinazojitegemea. Tayari Serikali imeshaagiza kufanyiwa kazi suala hili. Aidha, kwa upande mwengine, Sheria ya Mitaji ya Umma imo katika mchakato wa kufanyiwa mapitio na inatarajiwa kuwa eneo hili la malipo kwa wajumbe wa Bodi litazingatiwa na litafanyiwa kazi na shughuli hiyo inafanyika kupitia mradi wa *Public Finance Management Reform Progromme*.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kutokana na majibu mazuri ambayo Mhe. Waziri, ameyajibu. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuwalipa wafanyakazi hao wa Bodi kwa kutumia uwiano mmoja ambao unaweza kulingana na malipo yao yote hayo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba arudie suala lake sijalipata vizuri.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hidaya, rudia suala lako.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Waziri, nimeuliza hivi kwamba je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuziweka sawa hizi Bodi zote kwa kupitiwa wakurugenzi wao ili kuwa na uwiano mmoja tu wa malipo yao yote, ikaondoka hii kuwa wengine wana mishahra mikubwa wengine wana maposho madogo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Kama nilivyosema katika jibu mama kwamba hivi sasa Serikali imeshaagiza suala hilo lifanyiwe kazi na linafanyiwa kazi kupitia mabadiliko ya Sheria ya mitaji ya umma *Public Investement Act*. Tunaifanyia mapitio na sheria hiyo itakuja hapa Barazani na Waheshimiwa Wajumbe, mtapata nafasi ya kuichangia. Lakini ni moja ya pungufu ambalo Serikali imeshaliona na tuna haja sasa hivi ya kuangalia jinsi gani tunaweza tuka-*harmonise* maposho wanayopata wajumbe wa Bodi mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, wakati Wahesimiwa Mawaziri wanajibu masuala hapa mnazungumza sana, minong'ono imekuwa mingi kwa kweli inawapa shida wengine ambao wanataka kusikiliza, labda wengine hawajaja kusikiliza ambayo yanayozungumzwa, lakini wale wanaotaka kusikiliza wanapata shida. Kwa hivyo, naomba sana Waheshimiwa, kama kutakuwa na mtu anataka kuzungumza jambo muhimu na mwenziwe mlango upo wazi, lakini mtupe nafasi hapa tufanye shughuli zetu. Nawashukuru sana.

Nam. 20

Juhudi za Kuwasaidia Vijana na Dawa za Kulevya

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Aliuliza:-

Vijana ndio uti wa mgongo wa Taifa letu lakini vile vile ndio nguvu kazi. Taifa lolote hutegemea sana vijana katika kuleta maendeleo. Hata hivyo sasa kumekuwepo na wimbi kubwa la utumiaji wa dawa za kulevya ambapo vijana wengi hupoteza muelekeo na kupelekea taifa kupoteza nguvu kazi.

(a) Je, Serikali inachukuwa juhudi gani kuwanusuru vijana hao.

(b) Katika kuwarekebisha tabia vijana ambao wameshaathirika na madawa ya kulevya, Serikali imeshaanzisha nyumba ngapi za kurekebisha tabia (*Sober House*) ambazo zinamilikiwa na Serikali kupitia Wizara husika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Alijibu:-

Bismilahi Rahmani Rashim. Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naomba niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma anaendelea kutupa pumzi zake na asubuhi hii tukakutana hapa tukiwa katika hali ya uzima. Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibu swali naomba kwa ruhusa yako naomba uniruhusu niweze kusema neno.

Mhe. Naibu Spika: Umeniomba, niache nikuruhusu Mheshimiwa. Nakuruhusu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa dhati kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Rais Ali Muhammed Shein, kwa uwaminifu wake kwangu. Naomba nichukue nafasi hii kumuahidi Mhe. Waziri, kwamba sitomuangusha nitajitahidi kadri ya uwazo wangu, akili yangu, busara zangu.

Vile vile, Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuwaomba Waheshimiwa wa Baraza lako tukufu naomba mashirikiano yao na maelekezo yao, niko tayari kukosolewa nikiamini kwamba tunajenga nyumba moja na hakuna mkamilifu isipokuwa mwenyewe (*S.W*).

Baada ya maneno hayo machache Mhe. Naibu Spika, sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis Nafasi za Wanawake suala lake namba 20, lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba, Vijana ndio uti wa mgongo wa Taifa letu na vile vile ndio nguvu kazi na Taifa lolote hutegemea sana vijana katika kuleta maendeleo. Hata hivyo, kumekuwepo na wimbi kubwa la utumiaji wa dawa za kulevya ambapo vijana wengi hupoteza muelekeo na taifa kupoteza nguvu kazi.

Mhe. Naibu Spika, suala la dawa za kulevya kisheria na kisera linasimamiwa na Tume ya Taifa ya Kuratibu na Udhibi wa Dawa za Kulevya, ambayo iko chini ya Ofisi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwa hivyo, kifungu (b) cha swali hili lililoulizwa linahusu Tume hiyo. Kifungu (a) cha swali nililoulizwa linahusu Wizara ninayoiongoza. Naomba kujibu kifungu (a) cha swali hilo kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara kwa upande wake inachukua juhudi mbali mbali za kuwanusuru vijana hao kwa kuandaa mikakati mbali mbali ya kuwawezesha kuepukana na jambo hilo. Mikakati hiyo ni kama ifuatavyo:-

i. Kutoa elimu juu ya athari za dawa za kulevya kwa kutumia mbinu tofauti kwa jamii ikiwemo kuchapisha vitabu na mabango ya kuelimisha jamii dhidi ya dawa za kulevya.

Wizara yangu na Wizara inayoshughulikia masuala ya vijana (SMT) tumekubaliana kuufanya ujumbe wa Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya kuwa agenda ya kudumu kila mwaka katika ujumbe wa Mbio za Mwenge wa Uhuru. Kutokana na makubaliano hayo, kauli mbiu ya mbio hizo mwaka 2015 ilihusu *"UTEJA WA DAWA ZA KULEVYA UNAZUWILIKA NA KUTIBIKA, CHUKUA HATUA"* na kauli mbiu ya mwaka 2016 ina sema *"TUJENGE JAMII NA UTU WETU BILA DAWA ZA KULEVYA".*

ii. Wizara kwa kushirikiana na *UNFPA* tunatoa mafunzo ya Stadi za Maisha kupitia mkusanyiko wa Vijana. Mafunzo hayo yanatolewa kwa kupitia makongamano mbali mbali ambayo yanahusisha Taasisi zote za vijana ikiwemo zisizo za Serikali Unguja na Pemba. Vijana hao wanapewa mafunzo mbali mbali ikiwemo ushauri nasaha wa kutunza afya zao kwa ujumla (Athari za mimba za utotoni, UKIMWI, dawa za kulevya, pamoja na ajira kwa ujumla). Mwaka 2015 jumla ya vijana 5,000 – Unguja na 2,000 Pemba walipatiwa mafunzo hayo.

iii. Vile vile, Wizara inawahamasisha vijana kujiunga katika vikundi mbali mbali vya ushirika ili kupatiwa mafunzo na kuwaunganisha na fursa zilizopo zikiwemo za mikopo nafuu ili kupata mitaji ya kuanzisha na kuimarisha shughuli zao za uzalishaji ili kujipatia ajira.

iv. Wizara imeandaa Sera ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2005 na kufanyiwa mapitio mwaka 2015 ili iendane na wakati. Sera imebainisha majukumu ya vijana wenyewe, jamii, Taasisi zisizo za Kiserikali, Sekta binafsi na washirika wa maendeleo katika kumnusuru na kumuendeleza kijana.

v. Wizara imeandaa sheria ya kuanzisha Baraza la Vijana kwa lengo la kuwashirikisha vijana katika kupanga, kutekeleza mipango mbali mbali ya maendeleo.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante Mhe. Naibu Spika, katika majibu mama ya Mhe. Naibu Waziri, amesema kuwa Wizara inachukua juhudi mbali mbali na mikakati mbali mbali ya kuwanusuru vijana hao. Ningemuomba akanieleza vizuri ni mikakati ipi iliyochukuliwa, hiyo mikakati mbali mbali ni mikakati ipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sama Mhe. Naibu Spika, mikakati inayochukuliwa ili kuwanusuru vijana ni kama ivuatavyo; Kutoa elimu juu ya athari za dawa za kulevya kwa kutumia mbinu tofauti kwa jamii ikiwemo kuchapisha vitabu na mabango ya kuelimisha jamii dhidi ya dawa za kulevya.

Mhe. Waziri wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, naomba kuongeza majibu.

Kwanza nijibu swali (b) la msingi ambalo Mhe. Waziri, amesema linahusu Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kujua kwamba serikali inachukua juhudi gani katika kuwanusuru vijana na madawa ya kulevya.

Serikali tayari imejenga kituo kikubwa cha kurekebisha watu wanaoathirika na matumizi ya madawa ya kulevya katika eneo la Kidimni Wilaya ya Kati. Kituo hicho kipo tayari na hivi sasa kinatarajiwa kuanza kazi, kiasi cha jumla Shilingi bilioni 1.4 zimetumika kwa kazi hiyo.

Hata hivyo, serikali inachukua jitihada za ziada kuzisaidia *Sober Houses* 12 kwa kuzipatia milioni moja unusu kwa ajili ya kujiendeleza kila mwaka. Kwanza serikali inawapongeza sana wale walioanzisha *Sober Houses* na bado tutaendelea kuzisaidia *Sober Houses* hizo ili ziweze kutoa huduma bora kwa wananchi wetu na kushirikiana nao ili kupambana na suala hili la madawa ya kulevya. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri.
Katika majibu yake mama aliyojibu ametueleza kwamba wamechukua jitihada mbali mbali ya kuweza kuwasaidia vijana. Sasa hivi nataka kumuuliza ili kupata kujua, je, Wizara imewahamasisha vijana wangapi katika kujiunga na vikundi mbali mbali vya ushirika Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, Idara ya Vijana kwa mwaka 2016 imepanga kushajihisha vikundi 73 vya vijana Unguja na Pemba. Kwa robo ya kwanza ya utekelezaji imeshajihisha vikundi 23, ikiwa Pemba ni vikundi 13 na Unguja ni vikundi 10. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Wazee mtanisamehe, nawapa vijana suala lao hili.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kutuona vijana wako. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, kwenye jibu lake mama alisema kwamba vijana 500 wamepatiwa mafunzo. Naomba Mhe. Waziri, anambie ni vijana wangapi wanaume na wangapi wanawake ambao kuwa walipatiwa mafunzo hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, katika majibu yangu mama nimesema kuwa vijana 500 ndio waliopata mkopo huo, lakini analolitaka yeye Mhe. Viwe, ni kwamba wanawake ni wangapi na wanaume ni wangapi.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumwambia Mheshimiwa kwamba, takwimu ya wanawake ni wangapi na wanaume ni wangapi kwa sasa hivi sina, naomba Mheshimiwa nimjibu kwa maandishi.

Nam. 10

Kuanzishwa Shahada ya Kwanza - Pemba

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Aliuliza:-

Katika kuimarisha suala la elimu nchini, serikali imeamua kwa makusudi kutanua elimu ya vyuo vikuu Kisiwani Pemba baada ya kuanzisha tawi la *SUZA* katika chuo cha Benjamin William Mkapa huko Mchangamdogo.

Je, ni lini Serikali itaanzisha ngazi ya Shahada ya Kwanza ya Ualimu, Uongozi na Utawala (*Degree*) ili walimu walioko Pemba waweze kujiendeleza kielimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo la Mgogoni swali lake namba 10. Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa kilichopo Mchanga mdogo, Pemba ni tawi la Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*). Chuo hicho cha Ualimu kimeunganishwa na *SUZA* kwa madhumuni ya upatikanaji wa elimu ya juu katika sehemu mbali mbali za nchi yetu. Kwa kuanzia Kampasi ya Mchangamdogo imeanza kwa kutoa mafunzo ya miaka 3 ya Stashahada ya ualimu wa masomo ya sayansi. Mafunzo hayo yanatolewa kwa waombaji wote waliotimiza sifa bila ya kuangalia sehemu wanayotoka waombaji kama ilivyo taratibu za Chuo.

Mafunzo ya ualimu yametolewa kutokana na mahitaji makubwa ya walimu wa skuli zetu za Sekondari kwa masomo ya Sayansi. Mafunzo ya fani nyengine yatatolewa baadae kwa kadri ya mahitaji ya taifa yatakavyojitokeza. Kwa hivi sasa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar hakijakusudia kuanzisha mafunzo ya Shahada ya Uongozi na Utawala katika elimu huko Pemba. Mafunzo ya Stashahada ya fani hiyo yanatolewa kwa waombaji wote wenye sifa katika Kampasi ya Unguja. Ahsante.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali langu la nyongeza, pamoja na majibu mazuri aliyotoa naomba nimuulize.

(a) Kwa kuwa utafiti ni sehemu kubwa katika Vyuo Vikuu, Katika Chuo chetu Kikuu ni tafiti ngapi zilizofanywa ambao zinazohusu maslahi ya nchi yetu hii na kutolewa taarifa.

(b) Je,Wizara yake imewahi kufanya bajeti ya kuhusu utafiti kwa Vyuo Vikuu vya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika,

(a) Ni kweli kazi kubwa kabisa ya chuo kikuu chochote duniani ni kufanya utafiti licha ya kusomesha na shughuli nyengine za kufanya *consultancies*. Kwa hivyo, kila Chuo Kikuu ni wajibu wake kufanya tafiti na tafiti hizo zinafanywa kwa madhumuni mbali mbali. Kuna tafiti zinazofanywa na wanafunzi wenyewe katika kukamilisha masomo yao, kuna tafiti nyengine zinafanywa kwa ajili ya *consultancies* na kuna tafiti nyengine zinafanywa kwa miradi mbali mbali. Ni vigumu kuorodhesha tafiti isipokuwa useme maalum tafiti vilizofanywa kwa kitu fulani, tafiti lizofanywa kwa jambo fulani hiyo inawezekana, lakini katika ujumla wake inakuwa ni vigumu, kwa sababu tunaweza kuingiza mpaka zile tafiti ambazo wanazifanya wanafunzi kazi ndogo ndogo.

(b) Kuhusu bajeti, kila Chuo Kikuu kwa kuwa hii ni kazi ya msingi utafiti lazima kutakuwa na bajeti yake, iwe Chuo Kikuu cha Taifa au vyuo vyengine binafsi kunakuweka na bajeti ya kufanya shughuli za utafiti.

Mhe. Masoud Abrahmani Masoud: Mhe. Naibu Spika, kwanza nishukuru kwa kupatiwa nafasi hii, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri wa Elimu, swali la nyongeza. Chuo cha *SUZA* cha Benjamini William Mkapa kilichopo Mchangamdogo, Walimu pamoja na wafanyakazi bado hawajapata stahiki zao za kuwa *SUZA* mpaka leo. Je, ni lini watapatiwa stahiki zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ni kweli wafanyakazi waliopo katika Kampasi ya Mchangamdogo ambao jumla yao ni 14 bado wajapata stahiki zao, stahiki zao watapata wakati wowote baada ya taaratibu za uhamisho kukamilika, na taratibu hizo zimeshaanza tunatarajia si muda mrefu zitakamilika.

Nam. 91

Utolewaji wa Elimu Mjumuisho Katika Skuli Mbali Mbali

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Aliuliza:-

Elimu ndio msingi wa maisha kwa binaadamu, hivyo binaadamu anatakiwa kupatiwa elimu bila kubaguliwa, bila kujali kuwa huyu ni mtu mwenye ulemavu au asiye na ulemavu, wote wana haki sawa ya kupatiwa elimu. Kama vile Katiba ya Zanzibar, Ibara ya 25 (1) inayotoa haki za lazima na uhuru wa binaadamu.

(a) Kuna skuli maalum ambayo iliyotengwa kwa ajili ya kutoa elimu ya Mjumuisho lakini cha kusikitisha kwamba elimu hiyo katika hizo skuli haisomeshwi kabisa.

(b) Je, Serikali kupitia Wizara ya Elimu ina mpango gani katika kuiboresha elimu hiyo ili watu wenye ulemavu waweze kuipata.

(c) Je, ni lini elimu hiyo itaanza kutolewa ili watu wenye ulemavu wapate kufaidika na elimu hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo la Bububu swali lake namba 91, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

Kwanza naomba kutoa maelezo ya ufafanuzi kama hivi ifuatavyo:-

Elimu Mjumuisho ni mbinu ya kufundisha inayomuwezesha mwalimu kufundisha watoto wote kwa pamoja kwa mbinu inayowawezesha wanafunzi wote kupata elimi kwa kuzingatia mahitaji yao. Hivyo, Elimu Mjumuisho si somo bali ni njia ya kufundishia. Baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi kama ifuatavyo:-

a) Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo kwa walimu ili walimu wote waweze kutumia mbinu ya Elimu Mjumuisho katika kufundishia na kuelewa mahitaji ya watoto wote bila ya ubaguzi. Pia, Wizara yangu itaendelea kubadilisha mazingira ya skuli ili yaweze kuwa mazingira rafiki kwa wanafunzi wote wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji

maalum. Mahitaji hayo ni kama kujenga *ramps* za kuwawezesha watoto, wanaotumia vigari kuweza kuingia kirahisi katika majengo ya skuli na pia kuwepo vyoo vipana vitakavyowawezesha kuingia na vigari vyao. Aidha, wizara yangu itaendelea kununua vifaa mbali mbali kama vile *Brailler* na vifaa vya usikivu ili wanafunzi wenye mahitaji maalum wawe na vifaa vya kusomea.

b) Wizara itaendelea na juhudi ya kuandaa mazingira mazuri ya kutoa Elimu Mjumuisho kwa kukamilisha Rasimu ya Sera ya Elimu Mjumuisho, kuandaa *programmes* mbali mbali za elimu kuanzia elimu ya maandalizi ambazo zitazingatia mahitaji ya Elimu Mjumuisho na kuendelea kutoa mafunzo ya cheti na Stashahada ya Elimu Mjumuisho katika Vyuo vya Ualimu na Chuo Kukuu cha Taifa cha Zanzibar.

c) Elimu Mjumuisho itaendelea kupewa mkazo na ifikapo mwaka 2020 skuli zote za Serikali zitakuwa zinazingatia kutumia mbinu za Elimu Mjumuisho.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Mhe. Naibu Waziri. Katika jibu lake amezungumza kwamba Elimu Mjumuisho sio somo lakini ni mbinu mjadala ya kufundishia. Je, kwa sasa hivi ni walimu wangapi wamewafundisha hiyo mbinu ya kufundishia ili waweze kuitoa elimu hiyo kwa ufanisi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa swali hili linahitaji takwimu naomba kulijibu baadae kwa maandishi.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, napenda kumuuliza swali dogo la nyongeza. Baadhi ya walimu tayari wameshapata mafunzo ya Elimu Mjumuisho, lakini mpaka hivi sasa hawasomeshi mafunzo yale. Je, Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba mafunzo yale ya Elimu Mjumuisho wanapewa wanafunzi maskulini.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ni kweli baadhi ya walimu wameshapata mafunzo ya Elimu Mjumuisho na wengine wana vyeti na wengine wana Stashahada. Lakini kama tulivyosema Elimu Mjumisho ni mbinu kwa maana kwamba darasa ambalo amepewa mwalimu limewaingiza wanafunzi wenye mahitaji tofauti mbali mbali darasa hilo mwalimu anatumia mbinu hiyo ya Elimu Mjumuisho. Lakini baadhi ya

madarasa utakuta watu waliopo ni wa aina moja.Kwa hivyo, hao wana mbinu yake. Lakini nataka nifafanue zaidi, Elimu Mjumuisho haiwahusu watu wenye ulemavu peke yao hata wale ambo ni *best intelligent* nao pia wanaingizwa katika Elimu Mjumuisho na kwa sababu nao wana mahitaji yao maalum.

Kwa hivyo, kwa ufupi mbinu hii ni mbinu ambayo ina *balance* wanafunzi kwa mujibu wa mahitaji yao. Sasa sisi huku katika Wizara hatuna taarifa kama hawasomeshi, lakini taarifa tulizonazo sisi kwamba walimu wote ambao watakuwa ndani yake kuna wanafunzi hao basi wanatumia mbinu hiyo. Ahsante.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la mwisho la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, napenda nimuulize swali la nyongeza. Kuna tatizo kwa baadhi ya walimu ambao wanamaliza hii Elimu Mjumuisho kule Chuoni wanaporudishwa maskulini wanakataa kusomesha yale madarasa ya Elimu Mjumuisho kwa visingizio vya kwamba lile darasa kutokana na hali zao wale wanafunzi wengine linakuwaje. Je, Serikali kutokana na tatizo hili inawachukulia hatua gani wale walimu ambao wamepata elimu na wakashindwa kwenda kuifanyia kazi kule wanakokwenda.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Elimu baada ya mwalimu kurejea masomoni inampangia kazi na tunasisitiza kwamba mwalimu afanye kazi kwa mujibu wa taaluma yake aliyoisomea.Tunaendelea kuhimiza na tutaendelea kuhimiza na tumeshawaambia walimu kwamba, mwalimu tutampangia kazi kwa mujibu wa fani yake aliyosomea. Lakini hata wale ambao tunawapa mafunzo ya semina ndogo ndogo na wao pia tunawaeleza kwamba kile walichojifunza tutafatilia. Kwa hivyo, niseme tu kuanzia sasa hakutakuwepo na mwalimu hata mmoja atakaesameheka kusomesha somo au fani ambayo amesomea kwa kiwango cha juu. Ahsante sana.

Nam. 110

Uajiri wa Wanafunzi Wanaomaliza Masomo ya Ualimu

Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Aliuliza:-

Naipongeza Serikali kwa kuanzisha vyuo vingi vya uwalimu hapa Zanzibar ili vijana wetu waweze kujipatia taaluma ya uwalimu, lakini cha kusikitisha sana

kuna vijana ambao wamesomeya uwalimu ngazi ya cheti tokea 2008 mpaka leo hawajaajiriwa.

(a) Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuweza kuwaajiri vijana hawa japo kuwa hivi sasa wanaohitajika zaidi ni walimu wa masomo ya sayansi.

(b) Ikiwa vijana hawa wataendelea kukosa ajira hatuoni msongamano mkubwa wa foleni ya uwalimu umezidi kukuwa na kwa kuwa vijana ndio nguvu kazi ya taifa hili tutawasaidia vipi vijana wetu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:Alijibu:-

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Viwe Khamis Abdalla Mwakilishi wa Nafasi za Wanawake swali lake namba 110 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Wizara imezipokea pongezi za Mheshimiwa Mwakilishi kwa kuanzisha vyuo vingi vya mafunzo ya Ualimu. Kwa hivi sasa mafunzo ya Ualimu yanatolewa na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na tawi lake la Kampasi ya Benjamin William Mkapa huko Mchangamdogo, Pemba, Chuo Kikuu cha *Al-Sumait* na Chuo cha Kiislam, Unguja na Micheweni Pemba.

Vyuo hivi vinatoa mafunzo katika ngazi ya Cheti hadi Shahada ya Ualimu wa masomo mbali mbali na kumesaidia katika kuongezeka idadi ya walimu waliohitimu kwa baadhi ya fani. Pia, wapo baadhi ya walimu wanaojiunga na masomo ya Shahada ya ualimu katika vyuo vikuu vilivyoko Tanzania Bara. Aidha, ni kweli kuwa baadhi ya walimu waliohitimu mafunzo ya ualimu cheti mwaka 2008, hadi hii leo hawajaajiriwa. Baada ya maelezo hayo, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

a) Napenda nikiri kwamba katika baadhi ya fani kuna walimu wengi waliohitimu kuliko mahitaji katika skuli zetu na fani nyengine zina wahitimu wachache. Kwa hivi sasa, kipaumbele cha ajira kipo katika walimu wa masomo ya sayansi na hesabati. Nawashauri walimu ambao hawajaajiriwa na wamehitimu mafunzo ya cheti cha ualimu, wajiendeleze zaidi kwa kujiunga na masomo ya Stashahada ya ualimu katika fani zenye mahitaji makubwa.

b) Uajiri wa walimu utategemea kuwepo kwa mahitaji na nafasi za kazi za ualimu katika skuli zetu na sio kuwepo kwa wahitimu waliosomea ualimu. Hata hivyo, kutokana na kuongezeka kwa wanafunzi na ufunguzi wa skuli mpya, wizara yangu inatarajia kuajiri baadhi ya walimu kulingana na nafasi zilizopo. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, wizara inatarajia kuajiri walimu 900 wapya wakiwemo wa sayansi na wa sanaa katika masomo ambayo yana uhaba mkubwa wa walimu.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kumuuliza maswali mawili Mhe. Naibu Waziri (a) na (b).

(a) Kuna vijana ambao wamemaliza kusomea ualimu na sasa hivi wanajitolea katika skuli mbali mbali Unguja na Pemba. Je, vijana hawa inapofika mwisho wa mwezi kuna chochote ambacho kuwa wanapatiwa na Wizara hii ya Elimu.

(b) Kwa kuwa vijana hawa wapo wanajitolea na wameonesha uzalendo wa nchi yao, zinapotokea ajira ni kipaumbele gani ambacho wanapewa hawa vijana ambao kuwa wanajitolea katika nafasi za ajira.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Viwe, kama ifuatavyo:-
(a) Kwa kuwa vijana hawa wanajitolewa, Wizara ya Elimu haina nafasi yoyote ya kutoa sabuni kwa vijana hawa, badala yake katika skuli ambazo zimewachukua kwa ajili ya kujitolea wao ndio wanapaswa kutoa sabuni kwa vijana hawa.

(b) Suala la ajira ni suala ambalo ni la kitaifa, haliwahusu tu vijana wanaojitolea. Kwa hivyo, zinapopatikana nafasi tupu za kazi taratibu za kiserikali za ajira zinafuatwa; nazo tangazo la kazi linatoka, sifa zinazohitajika katika kuomba kazi hiyo, na kwa maana hiyo Watanzania wote au Wazanzibari wote wanaruhusiwa kuomba nafasi, anayejitolea na asiyejitolea. Kwa hivyo, hakuna upendeleo maalum kwa wanaojitolea. Ahsante.

Nam. 7

Maendeleo ya Boti za uvuvi zilizotolewa kwa Wavuvi

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupitia Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, ilitoa boti nyingi za uvuvi Unguja na Pemba, lakini hadi sasa boti hizo nyingi hazionekani.

Je, Mhe. Waziri, boti hizo hivi sasa zinaendelea vipi kwa shughuli za uvuvi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele swali lake kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ilitoa boti kwa wavuvi kwa lengo la kuwasaidia wananchi wetu kujiimarisha kiuchumi na kuendeleza uvuvi kupitia mradi wa *TASAF*. Kutokana na ufuatiliaji uliofanywa zaidi ya asilimia 60 za boti hizo zinaendelea kuvua kama ilivyokusudiwa na wavuvi wanajiendeleza vizuri. Hata hivyo, baadhi ya boti zimeuzwa na nyengine kuharibika. Wavuvi waliopewa vyombo hivyo na kuviuza wamekwenda kinyume na malengo ya Serikali ya kuwainua kiuchumi wavuvi na wananchi kwa jumla. Kutokana na hali hiyo, Wizara inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu ambao wengi wao wapo karibu na wananchi hao kushirikiana na wizara kusaidia kuwaelimisha wananchi wanaopata misaada kuitumia vizuri kulingana na malengo yaliyokusudiwa. Ahsante.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Serikali yetu ina nia njema na wananchi wake hasa katika makundi mbali mbali mojawapo likawa la wavuvi, na tunasema tu kwamba hata Mhe. Rais wetu Dr. Shein yuko mbioni kutafuta wahisani mbali mbali kuongeza nguvu katika uvuvi wetu wa maeneo makubwa zaidi ili kupatikana faida ya Serikali na wao wenyewe. Je, kwa kuwa hili limejitokeza na boti nyingi hazionekani na nyengine zilikuwa hazijulikani. Hivyo, Wizara itajitahidi vipi au ina mkakati gani pindi zikitokea hizo boti za maana za kwenda bahari kuhifadhiwa na kuwa salama ili zisipotee.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, Serikali inajitahidi kuwapatia wavuvi boti hizo, kwa hivyo, inaahidi kwamba kabla ya kutoa boti hizo wavuvi hao aidha tutawafungisha mikataba ama tutawachungulia taarifa zao zote ili lolote likitokezea tuweze kuwachukulia hatua.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize swali la nyongeza. Ni boti ngapi ambazo zilitolewa, lakini pia zilizouzwa ni boti ngapi na baada ya kugundulika zimeuzwa ni hatua gani ambazo zimechukuliwa kupitia Wizara.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, boti zilizotolewa kwa vile ni suala la takwimu, nitaomba nilijibu kwa maandishi lakini katika kuchukuliwa hatua hatujawachukulia hatua kutokana na kwamba mradi huu wa *TASAF* uko chini ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa hivyo, ninaahidi kwamba tutashirikiana na Ofisi hii ili kuweza kuwatambua na kuweza kuwachukulia hatua hiyo. Lakini suala la takwimu nitakuletea kwa maandishi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, naomba niongezee majibu ya Mhe. Naibu Waziri, ambaye amejibu kwa ufasaha kabisa. Suala la msaada ambao unaotoka Serikalini sehemu kubwa inategemea kabisa wananchi wenyewe wawe dhamana. Na wajibu wa Serikali ni kuwasaidia wananchi kupata huduma hii. Tusingependa kama Serikali mtu ambaye amesaidiwa halafu tukamshtaki kwa sababu hatukufunga nae mkataba kuweza kumshtaki kama hakufanya hivi. Mkataba wetu ilikuwa ni kuwasaidia na kuwapa huduma ile. Sasa tatizo linalotokea ni kwamba watu wengi kabisa baadhi yao hawakuwa waaminifu katika kutekeleza hivyo.

Hatua tunazozichukua ni zifuatazo:-

Kwanza, kuanzia sasa tutakuwa na utaratibu maalum wa kuhakikisha tunayempa chombo cha kufanyia kazi unachopewa na Serikali kuna mkataba maalum ambao atahakikisha kabisa anakitumia chombo hicho kwa madhumuni yaliyokusudiwa. Akenda kinyume na mkataba huo hatua zitachukuliwa. Hilo la kwanza.

Lakini la pili, ni kwamba kuna suala la boti kuvua bahari kuu, Serikali hivi sasa imekaa pamoja na wataotengenza maboti hapa Zanzibar ili kuona kwamba tunaweza kupata boti ambazo zinaweza kuvua kwenye bahari kuu. Cha msingi

katika kufanya kazi hiyo lazima tujenge uwezo wa wavuvi wetu ambao wanaweza kabisa kwenda kuvua katika bahari kuu.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Kwa ruhusa yako, naomba kuuliza swali la nyongeza. Huu ni mradi wa *MACEMP* ambao ulitoa boti na vifaa vyengine vya uvuvi, mradi ambao umetoa vifaa bila ya mpango wowote au bila ya kuzingatia hali halisi ya matumizi. Mimi ningemuomba Mhe. Waziri, akatujulisha labda ni kiasi gani cha mradi huu wa *MACEMP*, maana Naibu Waziri, amesema kwamba hafahamu boti ngapi pamoja na vifaa vingapi vilivyotolewa ila atatuletea kwa maandishi.

Lakini na mimi ningetaka kufahamu ni shilingi ngapi za mradi wa *MACEMP* tulipewa, hata kama kwa maandishi ni shilingi ngapi tulipewa na shilingi ngapi tulitumia katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza ni mradi wa *TASAF* na sio *MACEMP*. La pili, kuhusiana na gharama za mradi huu na shilingi zimetumika, nitamjibu kwa maandishi kama alivyosema mwenyewe.

Nam. 40

Ufuatiliaji wa Miche ya Mkarafuu Baada ya Kutolewa

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:-

Kwa kuwa serikali inagharamika kwa kutoa miche ya mikarafuu bure, kwa wakulima.

Je, serikali imejipaga vipi kuhakikisha kwamba miche iliotolewa inakua vizuri ili kufikia lengo la kuongeza uzalishaji wa karafuu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-
Mhe. Naibu Spika, mahitaji ya miche ya mikarafuu ni makubwa na yanayoongezeka siku hadi siku, hali hii imetokana na kuongezeka kwa thamani ya karafuu visiwani. Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imeandaa programu ya kuendeleza mikarafuu na katika uendelezaji wa programu hiyo wizara kwa kushirikiana na *ZSTC* inaendelea na mkakati wake wa kuotesha na

kuigawa bura miche 1,000,000 kila mwaka katika vitalu vyake Unguja na Pemba. Aidha, wizara imekuwa mstari wa mbele kushajihisha wakulima binafsi nao kuotesha miche ya mikarafuu kwa ajili ya matumizi yao na ziada kuwauzia wakulima ambao wanahitaji. Ahsante.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Mhe. Naibu Spika, ahsante naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa serikali hutumia pesa nyingi sana kwa kuhudumia vituo vya kuzalisha miche ya mikarafuu Unguja na Pemba, na kwa sababu miche ya jalbe hushika vizuri zaidi kuliko ile ya *nursery*, kwa utafiti wa wizara hii tunakuta kwamba kuna asilimia 37 ya miche inayopandwa ndio hushika.

Je, serikali ina mpango gani wa kuipata miche ya jalbe, yaani hiyo ya kung'oa na kuigawa kwa wakulima wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, miche ya *nursery* hata hiyo pia inashika ila inahitaji kipindi cha muda wa miezi 18 ili iweze kustawi vizuri. Vile vile, ningeomba sana Waheshimiwa wale ambao wanapata miche hiyo kuitunza na kuimwagilia maji kwani sasa hivi tunashajihisha zaidi kilimo cha umwagiliaji maji. Ahsante sana.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri, tunafahamu kwamba katika shamba la Kizimbani ambalo ni shamba la mikarafuu ni mikarafuu ambayo imechukua muda sasa hivi, na tunajua kwamba ile mikarafuu tayari imeshakuwa mikongwe kwa upevu.

Je, ni hatua gani ambazo zimechukuliwa na wizara ili kuekeza mikarafuu mengine kuweza kuziba yale mapengo ambayo yapo kwa ile mikarafuu ambayo imeshakauka na ile mengine ambayo inaendelea kukauka.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, ni kweli miche hiyo imekuwa haizai tunakubaliana na kauli yako uliyosema, lakini kama wizara imejiandaa mwaka 2016/2017 mpaka hadi mwezi wa Oktoba imeshaotesha miche 396,423, hiyo ndio jumla kuu. Kwa hiyo, tunajitahidi katika kuotesha miti hii ili tuweze ku-*replace* yale ambayo haizai tena. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba niongezee majibu ya Mhe. Naibu Waziri, ambayo ameyatoa kwa ufasaha kabisa.

Kwanza Mhe. Naibu Spika, ni kweli tunayo mikarafuu mikongwe na tuna mikarafuu ambayo yenye umri wa miaka saba mpaka minane. Mimi ningewaomba wakulima wote wa mikarafuu wazingatie mambo yafuatayo.

1) Mkarafuu ni mti ambao haupendwi sana kabisa kuchanganywa na mti mwengine, mizizi yake iko juu sana ukichanganya na vipando vyengine inakufa haraka sana.Hili ni jambo la kwanza kabisa lazima walizingatie.

2) Wale waliojitahidi kutumia mabotea wamefanikiwa sana kuweza kupanda mikarafuu mengi zaidi kuliko wale ambao wanategemea kuchukua miche yetu sisi wenyewe.

3) Niwaombe wale ambao wamechukua miche kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri, wajitahidi sana katika suala zima la kuitunza na kuipanda kwa wakati, ikitimia miezi 18 kwenye vitalu unahakikisha kabisa unapata mkarafuu ambao utastawi kama utauendeleza vizuri, ukifanya hivyo idadi ya mikarafuu itaweza kupanda.

Lakini kubwa Mhe. Naibu Spika, kuna tatizo kubwa sana la ujenzi wa majumba na mambo mengine, mikarafuu inakatwa kwa wingi na hili ni jambo moja tunahitaji kulizingatia kwamba huko tunapanda, lakini vile vile tuna kazi kubwa sana ya kukata miti pamoja na minazi na kadhalika. Nalo hilo ningewaomba wananchi tulizingatie sana.

N**am. 59**

Ubovu wa Barabara za Mtambile

Mhe. Mussa Foum Mussa - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inastahiki pongezi kwa kutujengea barabara za Mtambile – Kangani, Mtambile – Mwambe, Mizingani – Wambaa, na Kenya – Chambani, lakini kwa bahati mbaya hazikuwa na kiwango kizuri, na hivyo barabara hizo zimeanza kuharibika kwa kuchimbuka.

(a) Je, Mhe. Waziri, barabara hizi unazifahamu zilivyoharibika.

(b) Kuna mpango gani wa dharura wa matengenezo barabara hizo.

Mhe.Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 59, lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Ni kweli nazifahamu barabara hizo kama zimeharibika na tupo katika jitihada za kuzitengeneza kama jibu letu la (b) litakavyokuwa.

(b) Serikali ina mpango wa kuziongezea lami (*reseal*) barabara hizo kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara katika bajeti ya kila mwaka pale ambapo hali itakavyoruhusu. Aidha, wizara yangu kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara imekuwa ikizifanyia matengenezo ya kuziba mashimo yanayojitokeza kwenye barabara husika ili ziweze kupitika vizuri na kuzuia kuendelea kuharibika kama alivyosema Mhe. Mwakilishi haziko katika hali nzuri. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa barabara hizi zilipojengwa na hususan barabara ya Mtambile-Mwambe wananchi wengi waliharibiwa vipando vyao na muda umekuwa mkubwa karibuni miaka kumi bado wananchi hao hawajalipwa.

a) Je, serikali ina nia ya kuwalipa tena, na

b) Je, ikiwa nia hiyo ipo ni lini wananchi hao watalipwa pesa zao. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, ni kweli ni muda mrefu ambao wale waliokuwa wanataka fidia kwa vipando hawajalipwa, na sio kwa maeneo anayoyasema yeye bali kuna watu wa Gando, Konde wote hao wanatudai fidia na hivi sasa katika jitihada zetu na vile vile kutokana na ushauri tuliopewa tuhakikishe kwamba tunafanya tathmini baadae wahusika tunawalipa fidia kama vile wanavyostahiki. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kuweza kunipatia na mimi nafasi kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri, kweli barabara nyingi ni mbovu ingawa ni ndogo lakini inakuwa ni mbovu. Pia,

katika skuli ya maendeleo ya Ng'wachani ambapo tulifanya ziara ya kamati tulitembea kwenye skuli hii na tukaona ubovu ambao upo katika barabara hii inayoingia kwenye Chuo cha Maendeleo cha Ng'wachani.

Je, unajua ubovu wa barabara hii na kama kweli unajua ubovu wa barabara hii, vipi unaweza kutwambia kwamba barabara hii inaweza ikapatiwa matengenezo japo ya kwa njia ya fusi tu kwanza ili waweze kufaidika na ile barabara.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi nimpongeze sana kwa sababu hii ni mara ya pili kuniuliza swali hili, napenda kumuarifu kwamba, tunajua kuwa ile barabara ni mbovu japo ipo chini ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ lakini tunahakikisha kwamba barabara zote zile kwa kushirikiana na wizara husika basi tutazifanyia ukarabati pale hali inaporuhusu na awe na subra kwani lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha kwamba barabara zote zinapitika bila ya tatizo lolote lile.

Mhe. Makame Said Juma: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, katika jibu mama la Mhe. Naibu Waziri, amesema kwamba barabara ambazo zina mashimo huzibwa mashimo yale, lakini barabara ya Wete ambayo ni kongwe Pemba ina mashimo na kupelekea mpaka wapiti njia wa barabara ile kusumbuka na kupata usumbufu na kukosa kufika safari zao kwa wakati.

Je, ni lini mashimo yale ya barabara ile ya Wete yatazibwa ili kuwapa urahisi wananchi wanaopita katika barabara ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba barabara ile nayo ina mashimo kama alivyosema, lakini vile vile ajue kwamba sisi tunakwenda kwa mujibu wa bajeti na hali yetu ya kifedha tunajitahidi kadri inavyowezekana pale hali inaporuhusu basi barabara zile kuzifanyia marekebisho. Sasa mimi nimtoe wasi wasi kwamba suala lake hili nitalifanyia kazi ili kuhakikisha barabara sio ile tu bali barabara zote zile ambazo hivi sasa tushaanza kutia viraka basi na zile tunazitia viraka ili zipitike kwa urahisi. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, swali la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, nimekuwa na kilio cha muda mrefu kuhusu barabara yangu Konde/Msuka ambayo nimeshapewa ahadi mara nyingi hapa Barazani kwamba itafanyiwa

matengenezo hata ya awali ili wananchi wa Msuka waweze kufika angalau kwa vyombo.

Je, Mhe. Naibu Waziri, lini atanifanyia marekebisho hata ya kuziba viraka barabara ya Konde/Msuka ili wananchi waweze kufika angalau kwa gari. Mheshimiwa, naomba jibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Mwakilishi, kwa kuwa na hamu ya kutaka kuona kwamba jimbo lake nalo linapata maendeleo haraka hasa katika sekta hii ya barabara. Kama alivyosema mwenyewe kuna suala pia ameulizia katika kikao chetu hiki cha Baraza la Wawakilishi, lakini kwa vile suala hili lipo nitamjibu kwa ufupi tu hivi sasa. Ni kwamba ile barabara mimi mwenyewe nimeitembelea na tulipofika kule mpaka bandarini Msuka watu wametupa salamu kwamba wanaomba barabara ile tuitengeneze kwa sababu kabla ya hapo waliotokea washirika wakatoa fedha zisizopungua milioni 33 katika kuitengeneza ile barabara na ishaanza kuharibika. Nalichukua hili suala kwa vile ni ahadi hii tutaitekeleza awamu kwa awamu pale ambapo hali ya fedha itaruhusu. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Nam. 61

Ukosefu wa Kifaa cha Kupima Matumizi ya Pombe kwa Rubani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Rubani hutakiwa kukaguliwa na kifaa maalum kuangalia kama alitumia kiwango kikubwa cha pombe na ikithibitika haruhusiwi kurusha ndege siku hiyo. Na kwa kuwa kifaa hicho Zanzibar hakuna na kusababisha zoezi kutofanyika Zanzibar na Tanzania Bara.

(a) Je, ni kiwango gani cha pombe alichoamka nacho rubani ambacho haruhusiwi kurusha ndege.

(b) Je, ni lini kifaa hicho kitapatikana ili kuondosha hali ya wasiwasi ya kuwepo baadhi ya marubani kuwa na matumizi makubwa ya pombe na asubuhi kurusha ndege bila ya kuzingatia usalama wa wananchi na wao wenyewe.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 61 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Kanuni ya 57(1) ya "*Civil Aviation (Operation of Aircraft) Regulations*" inamkataza rubani kurusha ndege ndani ya masaa manane baada ya kunywa pombe, akiwa amelewa au akiwa na kiwango cha asilimia 0.04 ya uwiano wa uzito wa pombe katika damu yake.

(b) Kukiwa na sababu ya msingi kuthibitisha kwamba rubani amevunja au anatarajia kuvunja kanuni iliyotajwa hapo juu basi rubani atatakiwa kupimwa damu yake katika sehemu inayokubalika na Mamlaka ya Usafiri wa Anga (Hospitali ambayo kuna daktari maalum – *Aviation Doctor* ambae kwa Zanzibar anapatikana katika hospitali ya ZANZIBAR *MEDICAL GROUP* - SHANGANI na majibu yawasilishwe Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania kama ushahidi kwa kuchukua hatua za kisheria kwa muhusika.

Kanuni ya 184(2) ya "*Civil Aviation (Personnel Licensing) Regulations*" inasema kwamba, yeyote yule ambaye atakataa kupimwa ili kuonesha kiwango cha pombe kwenye damu yake au kuwasilisha majibu ya vipimo vyake kwa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania, Mamlaka itasitisha au kutengua leseni yake. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa zoezi hili halifanyiki Zanzibar na wala Tanzania Bara wakati kuna taarifa marubani wanaonekana saa sita za usiku kwenye mabaa au kwenye kumbi za starehe na asubuhi hurusha ndege na kuthubutu wakati mwengine hata kuondoka na viongozi wa kitaifa.

Je, ni lini kifaa hicho cha kugundua pombe kitanunuliwa na kuanza kuwakagua marubani wetu ili kuokoa usalama wa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka kumwambia kwamba sisi tunapojibu haya maswali tunajibu kitaaluma na wale ambao tunakaa nao kuyajibu maswali hawabahatishi, wao ni wataalamu wamebobea katika masuala haya na *DG* wangu alikuwa *Captain* wa Ndege anajua *ethics* zote za kazi yake. Napenda kumtoa wasi wasi kwamba sisi huu ni utaratibu uliowekwa wenyewe na Mamlaka ya Anga kwamba, hawa watu wapimwe katika hospitali maalum na

madaktari maalum ambao wamepasi maadili yote ya kidaktari. Daktari wetu yupo *Zanzibar Clinic* ambaye yeye tunahakikisha kwamba anakuwa mweledi na yuko katika maadili ya kazi na kazi hiyo kama inatokezea anaifanya.

Suala lake jengine anasema kwamba amewaona baadhi ya marubani usiku. Kama nilivyosema mwanzo wanaruhusiwa marubani nao kama binaadamu walivyo, starehe zao hatuwaingilii, lakini kabla ya masaa manane hatakiwi kunywa kiwango fulani cha ulevi nilivyokisema au dawa yoyote ile ambayo itaweza kumsababishia kizunguzungu. Kwa hiyo, hiyo ni *ethic* na madaktari wanajua kazi yao na vile vile hawa marubani wanajua kazi yao na kwamba, kutokana na kipato kikubwa wanachofanya katika kazi hii nina hakika kwamba watakuwa waaminifu na wahawatakubali kuhatarisha leseni ili wapoteze ajira zao. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri, ndege nyingi zinazokwenda Pemba mara nyingi huwa na rubani mmoja, na rubani ni binaadamu kama binaadamu mwengine.

Je, Mhe. Naibu Waziri, huoni kwamba hili ni tatizo la kwa abiria wale wanaoingia kwenye ndege ile litapotokea tatizo kwa rubani kuumwa au kupata tatizo jengine lolote.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, niko tayari kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake hili ambalo pia kesho litaulizwa, lakini nitajibu kabisa na kesho nitaomba yule muhusika aliyeuliza Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa ruhusa yake kama atanikubalia aliondoshe.

Sasa kwa utaratibu ndege zozote ambazo zina uzito usiozidi *pound* 12,000 sawa na Kilogram 5,500 zinaruhusiwa kuendeshwa na rubani mmoja. Kuna baadhi ya nchi ambazo kutokana na kipato chao wao ndio maana wanaweka marubani wawili. Sheria ya kwetu inamruhusu rubani kuwa peke yake kutokana na matakwa ya mwenye kumiliki ndege ile. Kwa nini wanafanya hivyo? Kwa sababu ile nafasi ya pili iwapo atamuweka rubani itabidi iongezeke gharama kwa mmiliki, kwa hivyo kuongeza nauli.

Kwa hiyo, hii kiutaratibu inakualika kabisa nataka tufahamishane kwamba hilo suala ni la kitaalamu kabisa na Mwenyezi Mungu anatujaalia kwamba mpaka sasa haijatokea ajali yoyote, licha ya kwamba ndege hizi zina rubani mmoja. Mhe. Naibu Spika, ahsante.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Katika majibu yake ya mwisho Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba gharama za kuongeza rubani mwengine kwa wamiliki wa ndege inakuwa ni kubwa, swali langu ni moja tu.

Gharama na roho za binadamu anaobeba kwenye ndege ile bora lipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo sisi tunakwenda kwa mujibu wa taratibu na sheria za Mamlaka ya Usafiri wa Anga na wao ndio wanazifuata sheria hizi za Kimataifa, kwamba ndege yoyote yenye uzito usiozidi *pound* 12,000 sawa na Kilogram 5,500 kwa sababu sisi sana tunatumia Kilogram, basi anaruhusiwa rubani kuwa mmoja. Kwa hiyo, hizo ni taratibu za kimataifa na sisi tunazifuata, isipokuwa kama nilivyosema mwanzo iwapo shirika, kanuni au sheria za nchi nyengine zinaona kwamba kuna umuhimu wa kuwa na marubani wawili basi wanafanya hivyo. Kwa hiyo na sisi tunafuata *regulations* au kanuni za kimataifa. Ahsante sana Mheshimiwa.

Nam. 100

Nyumba za Madaktari katika Hospitali ya Abdalla Mzee

Mhe. Bahati Khamis Kombo - Aliuliza:-

Hospitali ya Abdalla Mzee imemalizika na tutakuwa na madaktari wengi.

Je, Mhe. Waziri umejipanga vipi na nyumba za madaktari ili kuondosha kero kwa wafanyakazi wanaokaa mbali.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa ruhusa yako naomba sasa nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 100 kama hivi ifuatavyo:
Mhe. Naibu Spika, ni kweli ujenzi wa Hospitali ya Abdalla Mzee, Pemba umekamilika na ufunguzi wake utafanywa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein siku ya Jumamosi tarehe 26/11/ 2016 na wananchi wote mnakaribishwa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, suala la makaazi ya wafanyakazi ni jambo ambalo serikali imelipa umuhimu mkubwa na kuunda kamati maalum ya kushughulikia suala

hilo. Hivyo, kwa kuanzia wizara imekodi nyumba zenye hadhi na viwango na kuthibitishwa na kamati kwa ajili ya makaazi ya wafanyakazi hao.

Aidha, wizara imeazimia kujenga majengo manne ya ghorofa na kila jengo moja likiwa na ghorofa nne kwa ajili ya kuondosha kabisa tatizo la makaazi kwa wafanyakazi wa Hospitali ya Abdalla Mzee. Ahsante.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Mhe. Naibu Spika ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

(a) Katika kujibu swali lake la msingi amesema kwamba ana mpango wa kujenga majengo manne ya ghorofa. Je, Mhe. Waziri ni hatua gani ambazo zimeanza kuchukuliwa na wizara yake kuelekea kujenga maghorofa hayo.

(b) Ni eneo gani lililotengwa kujengwa maghorofa hayo katika Wilaya ya Mkoani. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, kwanza mipango madhubuti ambayo tumeshaipanga wizara kwa kushirikiana na Serikali Kuu ni kwamba tumeshapata kiwanja ambacho kipo Mkoani, kiwanja kikubwa, kizuri na kinakidhi mahitaji ya kujenga maghorofa manne.

La pili, ni kwamba hatua ambazo tumeshaanza kuzichukua ni kukagua majengo ambayo tumependelea yawe ni mfano wa majengo ambayo tutayajenga ya wakaazi wafanyakazi wa Hospitali ya Mkoani, tumeshayakagua kwa uongozi wa Mhe. Waziri wa Afya kwa kushirikiana na viongozi mbali mbali wa wizara majengo ambayo yapo Vitongoji, tuliomba ruhusa ya kuingia katika Kambi ya Jeshi tukaruhusiwa na kuingia kwenda kuyakagua na tukaridhika nayo. Baada ya hapo hatua tunayotaka kuendelea nayo baada ya ufunguzi ni kuhakikisha tunaandaa na kutengeneza ramani kwa ajili ya majengo hayo, pia kutafuta washirika wa kushirikiana nao katika kuhakikisha majengo hayo yanajengwa kwa haraka iwezekanavyo. Mheshimiwa ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Maryam Thani Juma: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

(a) Mhe. Naibu Waziri ni wafanyakazi wangapi wanaotarajiwa kufanya kazi katika Hospitali ya Abdalla Mzee mara baada ya ufunguzi.

(b) Katika hospitali hiyo, je, watakuwepo madaktari bingwa watakaotibu magonjwa mbali mbali yanayoshindikana katika Hospitali zetu za Pemba ili kuepusha usumbufu wa wananchi kusafiri kuja Unguja au Tanzania Bara.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, katika hospitali kubwa ambayo imejengwa kwa viwango ya Abdalla Mzee kwa kuanzia tunatarajia kuwa na wafanyakazi 227 wakiwemo madaktari 22. Lakini pia watasaidiana na madaktari bingwa rafiki zetu kutoka China madaktari wanane (8). Tunaamini kwamba huduma zote zitaweza kupatikana na bila ya usumbufu wowote. Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Pamoja na majibu yake mazuri lakini tumeshuhudia kwamba serikali inajitahidi kujenga majengo mazuri ya kijamii zikiwemo hizo hospitali, lakini matokeo yake serikali hushindwa kusimamia haya majengo na kupelekea kuharibika kwa muda mfupi.

Je, wizara imejipanga vipi kusimamia jengo hilo ambalo limejengwa, zuri, ni la mfano wa kimataifa ili lidumu na haiba yake hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, ni kweli serikali imeamua kujenga jengo hilo kwa gharama kubwa na limejengwa kwa ufadhili mkubwa wa ndugu zetu wa Kichina na inaahidi kwamba imeandaa miundombinu madhubuti ikiwemo ya ulinzi, kuwaelimisha wafanyakazi pamoja na wananchi kuhakikisha jengo lile linalindwa na linafanya kazi kama lilivyokusudiwa na kwa muda mrefu zaidi. Tunufaike sisi, wajukuu zetu, vitukuu na wataokuja mbele. *(Makofi)i*

Mhe. Naibu Spika: Nampa swali jengine la nyongeza Mhe. Tatu Mohamed Ussi, alinyanyuka lakini nimetaja jina jengine. Mhe. Tatu Mohamed.

Mhe. Tatu Mohamed Ussi: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kutokana na ubora wa vifaa na madaktari katika Hospitali ya Abdalla Mzee tunatarajia wananchi walio wengi kutoka Zanzibar watakwenda katika hospitali ile kwa ajili ya kupata huduma. Je, ni lini hospitali hiyo itaanza kutoa huduma kwa wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, mara tu baada ya ufunguzi siku ya tarehe 26/11/2016, siku ya Jumamosi baada ya Mhe. Rais wa Zanzibar

kufungua rasmi jengo lile basi tarehe 27/11/2016 jengo jipya la Mkoani linatarajiwa kutoa huduma zake rasmi na wananchi wote wanakaribishwa kwenda na matatizo yao. Wizara tayari imeshaandaa miundombinu ya kuhamisha madaktari pamoja na mambo mengine katika jengo hilo kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi. Mhe. Naibu Spika, ahsante.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana nimesimama hapa kwa Kanuni ya 63, nikirudi nyuma 42, sijui kama utaniruhusu niisome au utakuwa umeelewa kwa vile ni mzoefu wa sheria katika kitengo hiki.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa rudia tena sijakusikia vizuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, nimesimama hapa kwa mujibu wa Kanuni ya 63 kuhusu utaratibu, baadae natakiwa niseme kilichonisimamisha hapa ni Kanuni ya 42, sijui kama utaniruhusu niisome na kwa vile naamini wewe ni mzoefu wa sheria kwa kitengo hiki na ndio kufikia Naibu Spika. Sasa utaniruhusu niisome au niendelee na hoja yangu ninayotaka kuizungumza.

Mhe. Naibu Spika: Naifahamu naomba uendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kama unaifahamu Kanuni, kilichonisimamisha hapa ni hoja ya kujadili jambo la dharura kuhusu kukiukwa kwa sheria na taratibu za kupandisha viwango vya bei ya umeme kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi na kuleta athari kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa kwa mujibu wa kanuni hiyo una haki ya kuweza kuileta hoja mbele yetu, tuna muda wa saa moja tu kwa ajili ya kujadili, muda huo itaunganisha pamoja na hoja ambayo utaitoa pamoja na Wajumbe wengine ambao wataweza kuchangia. Kwa hiyo, kwa ruhusa yangu sasa naomba uwasilishe hoja yako.

Hoja ya Kujadili Jambo la Dharura Kuhusu Kukiukwa kwa Sheria na Taratibu za Kupandisha Viwango vya Bei ya Umeme

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana tena sana kwa kuniruhusu kuisoma hoja hii.

Hoja hii ya kujadili jambo la dharura imefanywa chini ya Kifungu cha 3 na 49(b) cha Sheria ya Kinga, Uwezo na Fursa za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Sheria Nam. 4 ya Mwaka 2007 na Kanuni ya 27 (1)(g) na 42 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Toleo la Mwaka la 2012 pamoja na vifungu vyengine vya sheria za kanuni vinavyowezesha.

Mhe. Naibu Spika, itakumbukwa kuwa mnamo Tarehe 31 Oktoba, 2016 wananchi wa Zanzibar ambao ni wapiga kura wetu walipata taarifa za ongezeko la bei ya umeme kwa asilimia 20 kupitia tangazo la Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwenye vyombo vya habari.

Mhe. Naibu Spika, kama Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Paje nikiwa nina wajibu kwa nchi yangu sina tatizo na juhudi zozote za serikali kuliwezesha Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO),* kuongeza wigo wa kukusanya mapato ili liweze kutoa huduma zake vizuri.

Mhe. Naibu Spika, naomba nirudie na Mhe. Waziri na Wajumbe wasikilize nia yangu hapa. Mwakilishi wa Jimbo la Paje nikiwa nina wajibu wa nchi yangu sina tatizo, narudia tena sina tatizo na juhudi zote za serikali kuliwezesha Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO)* kuongeza viwango vya kukusanya mapato ili kutoa huduma zake vizuri; sina tatizo hilo muhimu sheria zifuatwe na utaratibu.

Pamoja na hivyo, tangazo lililotolewa na Waziri kwa ongezeko la bei ya umeme limeleta manung'uniko kila pembe ya visiwa vyetu kutoka kwa wananchi wetu, kwa vile utaratibu wa kisheria na kutangazwa kupandishwa bei hizo hazijafuatwa na kutokufuatwa huko kumeathiri maslahi ya wananchi hao kwa vile ongezeko hilo limekuwa kubwa mno kulingana na hali ya maisha ilivyo hasa kipindi hiki kigumu.

Mhe. Naibu Spika, umuhimu wa kujadili hoja hii ya dharura ni muhimu katika Baraza hili la wananchi kwa kuwa:-

(a) Maslahi ya wananchi wetu yameathirika na yanaendelea kuathirika, kwa kuwa utaratibu wa ongezeko la bei ya umeme haukufuatwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati (*ZURA)* tuliyoipitisha katika Baraza hili Sheria Namba 7 ya Mwaka 2013, ambapo ilitakiwa na wao wananchi washiriki katika kutoa maoni yao. Sheria tumezitunga wenyewe na tumezipitisha wenyewe.

(b) Malalamiko ya wananchi yamekuwa makubwa kiasi ambacho wana hamu na wanataka kuona sisi Wawakilishi wao, tunaisimamia sheria ya *ZURA* inayosimamia taratibu zote na ongezeko la bei, huduma za umeme, maji na mafuta tanachukua hatua gani baada ya taratibu za sheria hiyo kutokufuatwa na wao kuathirika.

Mhe. Naibu Spika, chombo hiki kipo kwa niaba ya wananchi, na wananchi ndio walionituma.

(c) Baraza la Wawakilishi ndio chombo cha kikatiba kinachotunga sheria za nchi yetu kusimamia serikali na mnamo tarehe 8/04/2013 Baraza limetunga Sheria ya *ZURA* ambayo Mhe. Rais ameisaini tarehe 19/08/2013 ambapo *ZURA* tumeipa mamlaka ya kudhibiti huduma za nishati ya maji, mafuta na umeme ikiwemo udhibiti wa bei za huduma hizo. Baraza hili bado lina wajibu wa kusimamia na kuona kuwa kazi na uwezo wa majukumu ya kisheria ya *ZURA* yanafanywa na *ZURA* tu, kama sheria tuliyoitunga inavyotaka na si mtu mwengine yeyote.

Naomba nirudie tena.

(c) Baraza la Wawakilishi ndio chombo cha kikatiba kinachotunga sheria za nchi yetu, kuisimamia serikali na mnamo tarehe 8/04/2013 Baraza limetunga Sheria ya *ZURA* ambayo Mhe. Rais ameisaini tarehe 19/08/2013, ambapo *ZURA* tumeipa mamlaka ya kudhibiti huduma za nishati ya maji, mafuta na umeme ikiwemo udhibiti wa bei za huduma hizo. Baraza hili bado lina wajibu wa kusimamia na kuona kuwa kazi na uwezo wa majukumu ya kisheria ya *ZURA* yanafanywa na *ZURA* tu, kama sheria tuliyoitunga inavyotaka na si mtu mwengine yeyote.

Utaratibu ulivyokiukwa na athari kwa wananchi.

Mheshimiwa kila kitu nimeweka wazi kabisa hapa.

Mhe. Naibu Spika, Baraza la Wawakilishi limetunga kifungu cha 36 cha Sheria ya *ZURA* kinachotaka wananchi kushirikishwa katika kutoa maoni yao kabla ya bei mpya ya huduma za umeme, maji na mafuta hazijatangazwa. Jambo hili halijafanyika kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki, hali ya kuwa ipo kisheria matokeo yake bei ya umeme imepandishwa bila ya wananchi waliopandishiwa bei hizo kutoa maoni yao kama sheria inavyotaka.

Mhe. Naibu Spika, mamlaka ya kisheria ya kutangaza bei mpya ya umeme, maji na mafuta ni *ZURA* na sio waziri kwa mujibu wa kifungu cha 10 cha Sheria Namba 13 ya Sheria ya *ZURA*, ambapo wajibu wa waziri kutakiwa ushauri kwa mujibu wa sheria hiyo, nalo hilo limekiukwa, na waziri kuchukua mamlaka ya kutangaza *ZURA* kubakishwa na washauri tu, waziri alikuwa anatakiwa ashauriane na *ZURA* lakini *ZURA* ndio inashauriana na waziri, tunakwenda kinyume hapa.

Mhe. Naibu Spika, endapo kama kuna utaratibu wa kisheria wa kuachwa *ZURA* itoe matangazo na kuchukua maoni ya wananchi na kutoa mapendezo yao kabla ya bei mpya ya umeme kutangazwa malalamiko ya wananchi yasingekuwa makubwa, kwa vile ushiriki wao ungezalisha fikra ya namna bora za upandishwaji wa bei hizi bila ya kuleta athari kwa wananchi.

Hivyo, basi Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa kanuni ya 42 (10) ya kanuni za kudumu za Baraza la Wawakilishi jambo hili ni muhimu na linagusa maslahi ya wananchi, na utatuzi wake unategemea hatua zaidi kuliko zile za utekelezaji na utawala pekee. Naomba Baraza hili tukufu litoe maazimio yafuatayo.

Waheshimiwa Wajumbe hapa naomba mnisikilize kwa makini kwa maslahi ya wapiga kura wetu, na si yangu peke yangu haya.

(a) Kumtaka Waziri wa Maji, Nishati na Mazingira kusitisha mara moja utekelezaji wa tangazo lake la ongezeko la bei ya umeme hadi pale utaratibu sahihi wa kisheria utakavyofuatwa, kwa mujibu wa sheria za *ZURA* na Baraza hili kupitia kamati yake husika ya kisekta kusimamia na kuona utaratibu huo unafuatwa mpaka mwisho.

Hatukatai sheria tunatunga wenyewe humu ndani halafu tunazikiuka wenyewe. Tumeshuhudia humu tulikamata ng'ombe sheria haituruhusu bali tukaweka sheria tukakamata ng'ombe na hii tunatunza sheria, wenye mamlaka ni *ZURA*.

(b) Baraza hili lisimamie mamlaka yake ya kutunga sheria kwa kuitaka Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira isifanye majukumu ambayo Baraza hili limeyatunga kisheria na yatekelezwe kwa mamlaka nyengine.

(c) Zoezi la kutathmini ongezeko la bei ya umeme lianze tena upya kwa *ZURA* kuchukua jukumu lake kwa mujibu wa sheria na si waziri.

(d) Taarifa ya utekelezaji maazimio haya yawasilishwe ndani ya Baraza hili la Wawakilishi

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana kuna Wajumbe wameikubali hoja. Waheshimiwa Wajumbe nimepata wachangiaji 3 na nitakuwa makini kwenye muda, na muda huu utajumuisha mpaka michango ya Mawaziri majibu ya Mawaziri.

Baada ya kupita saa moja aliyetoa hoja ametumia dakika 5, baada ya kumalizika saa moja tutafanya maamuzi.

Kwa hiyo, nitaanza kwa mchangiaji wa mwazo kabisa ...

Utaratibu

Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mamshukuru pia Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa hoja yake ambayo ameileta.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Jaku Hashim ameleta hoja yake na amejikita kwenye sheria ya *ZURA*, Sheria namba 7 ya mwaka 2013 na ametaja vifungu vya sheria hiyo hiyo ya *ZURA*.

Mhe. Naibu Spika, na mengi ambayo Mhe. Jaku Hashim Ayoub ameelezea kuhusu kuvunja utaratibu wa sheria ya *ZURA* ndio maana akaja na hoja yake.

Sasa mimi naomba nitoe indhari kwa Baraza, kwamba na sisi tusiwe sehemu ya kuvunja utaratibu uliowekwa na sheria hiyo hiyo.

Mhe. Naibu Spika, sheria ya *ZURA* imeweka utaratibu wa kupokea malalamiko kwa watumiaji wa huduma, imeweka utaratibu mzuri kabisa kama Mhe. Jaku Hashim Ayoub angesoma kifungu cha sheria cha 38 kinaeleza jinsi gani ya malalamiko ya watumiaji huduma yanatakiwa yapelekwe kwenye Mamlaka. Si hivyo tu na kama maamuzi ya mamlaka wananchi hawakuridhika nayo wamepewa fursa pia ya kisheria kukata rufaa kwa bodi ya mamlaka na kama haitoshi pia wamepewa fursa ya kwenda mahakamani, huo ndio utaratibu wa kisheria.

Sasa leo sisi tunakaa hapa tunataka kuvunja utaratibu uliondikwa na sheria hiyo ya *ZURA* ambayo Mhe. Jaku Hashim ametoa vifungu vyake kwamba Mheshimiwa Waziri hakufuata.

Sasa mimi natoa indhari kama sisi tusiwe sehemu ya kuvunja utaratibu, ni vyema Mhe. Jaku Hashim akawaelekeza wananchi kufuata utaratibu wa kisheria na mwisho wa taratibu hizi ni mahakamani. Sasa kwa nini tuwe ni sehemu ya kazi ambayo si yetu Mhe. Naibu Spika.

Sasa ni vyema Baraza lako liamue vizuri Mhe. Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba tufuate utaratibu wa kisheria ambao umewekwa na kifungu cha 38 cha sheria hiyo hiyo ya *ZURA*.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mwanasheria Mkuu nimekuelewa sana na nafikiria kwamba hilo ni jambo ambalo tunalifanya tutajadili, lakini sio kwa msingi wa kuvunja sheria ni kwa msingi wa kutengeneza.

Kwa maana hiyo, nafikiri niwape nafasi na wengine lakini tukae tukijua indhari ambayo imetolewa na Mhe. Mwanasheria Mkuu. Kwa hiyo, hatuko hapa kuvunja sheria, tupo kwa kujadili na kuona muelekeo tutaelekea wapi.

Nafikiri haina haja ya kuzozana hapa, niwataje watakaochangia, watachangia lakini tukijua kwamba kuna maamuzi na maamuzi hayo hatutoweza kuvunja sheria zilizowekwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub nafasi yako imepita nawapa watu wengine ambao wameleta majina yao. Nitaanza na Mhe. Abdalla Maulid Diwani umeomba kuchangia hii hoja au umeshaghairisha.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Nitachangia Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Karibu.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii kuchangia hoja ya dharura ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa wananchi wa jimbo la Paje juu ya kadhia nzima iliyotukabili ya upandishwaji wa bei ya umeme bila ya kufuata utaratibu.

Pamoja na nasaha alizotoa Mwanasheria Mkuu tunaheshimu maamuzi yake na maelekezo yake tumeyapokea, lakini tuchukulie kwamba sisi tuko humu na tunasimamia Ibara ya 88 ya Katiba ya Zanzibar juu ya maslahi mazima ya Wawakilishi ndani ya chombo hichi. Tunaepuka sana Mhe. Naibu Spika, kuona kwamba tunakiuka yale ambayo yanayopangwa. Lakini kunakostahiki hakuna budi tuzungumze japo kwamba yanatokea matatizo tunapozungumza. Lakini siku zote ukweli utabakia ukweli, na kuzungumza tutazungumza kwa sababu ndicho tulichokigombania kupitia majimboni kwetu na tukapata nafasi kuingia kwenye chombo hichi kitukufu cha Baraza la Wawakilishi, kuwawakilisha wananchi wetu.

Sasa basi hoja ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub ni kweli ina mashiko kwa kutilia maanani kwamba sasa kila muda tunasikia matangazo mbali mbali kupitia *ZURA* juu ya suala zima la upandishwaji wa mafuta, dizeli, mafuta ya taa na petroli. Kila muda wanatangaza *ZURA* iweje kwa mafuta ifuate ule utaratibu lakini kwa umeme isifuate. Tayari ni tatizo kama alivyosimamia Mhe. Jaku Hashim, mwenyewe kwenye kipengele kilichovunjwa naomba ninukuu anasema"

36 (1) *"The Authority shall conduct public hearing for the purpose of carrying out of its functions at any public place to enable stakeholders to participate effectively and giveout their comments;*

Ni kweli tulizungumza kwamba tunapotaka mabadiliko yoyote juu ya kadhia hii ya upandishwaji huu wa bei, basi *ZURA* wao ndio watangaze bei baada ya kukaa na watumiaji. Gharama zetu tunajua juu ya maisha yetu jinsi yalivyo, na tumeona namna gani hii bei ilivyotamkwa tu, nafikiri tarehe 29 au 27 baada ya kupigwa makufuli na *ZRB* basi siku ya pili Mhe. Waziri anasema itakapofika tarehe 1 tunatangaza bei mpya asilimia 20 ya umeme. Jamani tumekosa nini sisi, bei asilimia 20 ni kubwa sana, tukitilia maana wananchi wetu wa hali ya chini wana maisha magumu, sisi wenyewe hapa ndani ya Baraza pengine wengi wetu hatulipi umeme mia juu ya mia.

Leo hii unatuongezea asilimia ishirini ya juu bila ya kufuata utaratibu, ukiukwaji kweli umepita. Sina nia mbaya katika serikali yangu na siku zote nitaisimamia serikali yangu, serikali niliyoiamini ya Chama cha Mapinduzi na sitobadilika katika hicho, lakini panapo ukweli juu ya kadhia yoyote ya nchi hii itabidi tuseme japo kuwa watu wa mbele wengine hamfurahii sisi tukisema. Lakini ni wajibu wetu kutokana na Katiba ya Zanzibar imetupa nguvu hizo, na vile vile ndani ya jengo hili tayari tuna dhamana kwamba tuseme yote bila ya kuhojiwa nje na chombo chochote.

Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa niseme hilo, na kwa sababu kadhia ya umeme kupandishwa bei bila ya kufuata utaratibu imepitikana lakini kumbuka kwamba sheria hii imepita humu humu, sheria namba 7 ya 2013 na Mhe. Rais, kaisaini. Sasa pengine waziri nikisema lugha ambayo haitomuudhi alikurupuka katika hili, basi aje akubali mbele yetu basi turekebishe zipite taratibu zile nyengine ili ziweze kutangazwa bei mpya ambazo zitakuwa na maslahi kwa Wazanzibari.

Nimesikia vile vile kuwa wenzetu wana sheria kama hii Tanzania Bara, siku Jumamosi wanaita *stakeholders* kwenda kuzungumza nao juu ya kadhia ya kupandishwa umeme, hata kule Tanzania Bara wale wenzetu wanafuata hii sheria na wameshatangaza si mara moja si mara mbili katika vyombo vya Habari na magazeti kuwaomba wananchi waende pale wanaita *"Clock Tower "* ya Mwenge wakazungumze juu ya kadhia hii ya upandishwaji wa umeme kwa Tanzania Bara.

Sasa mimi ningeomba tu na serikali yetu nayo ipite hizi taratibu, iwaite wadau ili wajadiliane nao wapange gharama kuangalia maslahi ya nchi hii kuweza kupandisha umeme. Kwa hiyo, mimi nisichangie mengi, mimi nilikuwa ni hayo tu niseme kutoa dukuduku langu juu ya kadhia ya kupandishwa umeme kiholela.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf Al-Wardy: *"Bismillahi Rahmaani Rahiim"* Mhe. Naibu Spika, ningeomba nijue dakika ngapi unatupa tuzungumze, ishirini au dakika ngapi.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa sijakufahamu vizuri.

Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf Al-Wardy: Ningependa kujua wakati wangu muda gani unanipa, dakika ishirini au ishirini na tano.

Mhe. Naibu Spika: Hapana hupati dakika ishirini na tano nitakupa dakika kumi tu hazizidi hapo.

Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu sana kunipa uzima na kutufikisha hapa sote.

Vile vile niwapongeze sana wananchi wangu wa jimbo la Chaani kwa kuniamini na kuhakikisha kwamba wamejitahidi mpaka nikafika hapa Baraza la Wawakilishi.

Mimi nitachangia hoja ambayo ameileta Mhe. Jaku Hashim Ayoub ya Mhe. Waziri kupandisha bei ya umeme kwa asilimia 20 na kukwepa au bila ya kufuata sheria.

Mimi ningeanza na mambo machache ambayo nitakayotaka kuzungumza. Tunafahamu kwamba sisi Wawakilishi tuna majukumu yetu na katika Ibara ya 88 katika Katiba ya nchi inatupa sisi nguvu za kuuliza maswali, kutunga sheria na mambo mengine karibu mambo manne.

Lakini cha ajabu zaidi kwamba tunapotaka kuleta hoja, tunapotaka kuzungumza ukweli basi baadhi ya Mawaziri hasa Waziri muhusika wa wizara hii tunayoizungumza ...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa humzungumzi mtu hapa unazungumzia hoja.

Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, tunachoomba sisi Wawakilishi tunapozungumza ubaguzi masuala ya kuitana *CUF* wakati tunapozungumza ukweli uishie humu humu, haya masuala kwamba tunazungumza halafu tunageuziwa kibao sisi hatutaki kuyaona Wawakilishi wa Baraza la Tisa.

Mawazari baadhi yao wana tabia hii ya kutukandamiza, unapozungumza ukweli kukugeuzia kibao kukuita *CUF* na mambo ya urangi na mambo mengine. Hili nasema dhahiri, kama nitakuwa nakwenda kinyume lakini Mhe. Waziri alilifanya hili kipindi cha nyuma.

Mhe. Naibu Spika, sisi tuko hapa kwa niaba ya wananchi, wananchi wanatutuma tunatumika na tuko hapa kwa ajili yao, sisi tumekuja hapa tumekamatishwa msahafu, hatujakamata kitabu cha mtu alichokitengeneza mtu, tumekamata kitabu cha Mwenyezi Mungu mtukufu, kitabu ambacho hatutakiwi tuseme uongo na kinatuapiza wenyewe, na ndio maana utakuja kukuta siku za mwisho kila mtu akimaliza madaraka humu ndani anaumwa na kivyake vyake tunajiuliza karogwa, hakuna cha kurogwa, uongo wetu na mambo tunayoyafanya ndio kinachofanya utugeukie msahafu mtukufu.

Sisi tutazungumza ukweli na hatumuogopi mtu, na wao wanaojifanya kwamba tukizungumza ukweli...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Nadir zungumzia hoja ya umeme ndiyo tunayozungumzia hapa. Nenda kwenye hoja Mheshimiwa muda wako utakwisha.

Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf Al-Wardy: Mimi muda wangu naujua dakika kumi utafika tu. Mimi naeleza hivi kwa sababu hili suala lipo Mhe. Naibu Spika, na tusitishane tuko hapa hawa hawa wanaofanya hivi.

Mimi natoa mfano mmoja tu wizara hii hii juzi imetangaza kwamba mambo ya ardhi itawafutia watu ardhi...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Nadir kaa kitako.

Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf Al-Wardy: Mheshimiwa naenda kwenye hoja.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Nadir kaa kitako, haki yako kwa kuchangia imeshakwisha.

Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante Mhe. Naibu Spika, lakini ukweli wameshausikia.

Mhe. Naibu Spika: Nilikwisha kukwambia tunachangia hoja hatuchangii malalamiko ya aina yoyote hapa, kwa leo ni hoja ya umeme ndiyo tunayoichangia. Kwa hiyo, muda wako uliobakia uchangie hoja ya umeme.

Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana, Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa sisi ndio watunga sheria na tunapotunga sheria lazima huko nje iheshimike, sio mtu mmoja akavunje sheria watu 88 kwa nchi nzima.

Mhe. Naibu Spika, kitendo cha Waziri kutangazia ndani ya vyombo vya habari kwamba atapandisha umeme kwa asilimia 20 kwa wananchi walio wanyonge na wanaotutuma ndani la jimbo langu la Chaani hawako tayari kwa suala hili, na tunaomba sana masuala kama haya yanapotaka kufanyika ahakikishe kwamba anafuata *procedures* asiwe yeye ndie kiongozi wakati kuna watu wana akili kuliko yeye, waliotengeneza haya mambo asidharau watu kwenye *Cabinet*, ahakikishe anashirikiana na watu kwenye kuangalia masuala yote anayotaka yeye ayafuate asikae tu akakurupuka kwenye TV kufuata umaarufu,

TV ina madhara yake, TV ina matatizo yake, unapokaa unapotaka kuzungumza kwenye TV ujue unaenda kuzungumza nini, huendi kuropokwa tu pale.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninachotaka kusema kwamba mambo haya ndio yanayosababisha mtu mmoja kuifanya serikali ionekane ina matatizo, kukifanya Chama cha Mapinduzi kionekane kina matatizo kwa mtu huyu mmoja, na tunaposema tutaonekana huyu katumwa, ukweli utabaki kuwa ukweli. Na nitasema kila siku hata anite nani, ukweli nitasema ukweli, na hapa hatujaja kufichana, hawa ndio wanaoharibu Chama cha Mapinduzi kusemwa vibaya nje, na dunia nzima sasa hivi inasema vibaya kwa mtu mmoja kwa kauli zake ambazo sio nzuri.

Namuomba sana mara ya pili anapotaka kuonekana kwenye *TV* au kwenda kwenye *TV* ahakikishe anachokiongea anakijua asifyetue fyetue.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: (Dimwa): Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja makini sana iliyowasilishwa na Mwakilishi makini wa Jimbo la Paje ndugu yangu Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze sana mtoa hoja na nataka niseme hoja hii imekuja ndani ya wakati wake.

Kwanza kabisa Mhe. Naibu Spika, kabla sijasoma au sijaendelea, kwa sababu sitachukua dakika nyingi, nataka uangalie tu Sheria yetu ya Kinga ikoje. Ukisha kuiangalia hii naanza kuendelea kusoma sasa.

Mhe. Naibu Spika, kama ungeniruhusu kwa wakati huu basi ningeomba leo nirudie lile neno la Maalim Haroun Ali Suleiman, katika siku yake ya bajeti niweze kuvaa ninja ili nisiwaone yeyote ambaye yupo mbele yangu, kwa sababu nimeangalia sana Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, lakini nikaangalia vile vile malengo ya Chama cha Mapinduzi kwenye Katiba yetu. Hakuna mambo haya yanayoweza kufanyika kama leo.

Mhe. Naibu Spika, hoja hii imekuja kwenye wakati wake, na ni hoja muhimu sana, kwa sababu wananchi wengi wa majimboni wanalalamikia tukiwemo na sisi wenyewe juu ya jambo zima la kupandishwa bei ya umeme.
Mhe. Naibu Spika, jambo hili unaweza ukaliona dogo sana lakini siyo kama munavyoliona, hili ni jambo kubwa sana. Mimi ninataka kusema labda bado

hatujajua tatizo liko wapi, kitu gani kinachotusibu hatujakijua, kitu gani tuelekee bado hatujakijua. Lakini hata ukusanyaji wetu wa kodi bado hatujaujua, tuanzishe vyanzo vingapi vya kodi bado hatujavijua. Ndiyo sasa tunaanza kuwadhulumu wananchi.

Nimesema hivi kwa sababu Mhe. Naibu Spika, baada ya kufungwa *ZECO* na *ZRB* ndiyo mambo haya yote yakaja. Lakini inasemekana wazi kuwa deni la *ZECO* kwa *TANESCO* limekuwa kubwa sana. Sasa ningetoa ushauri tu kwa Serikali yangu kuangalia ni mashirika mangapi ya binafsi ambayo yanadaiwa pesa nyingi za umeme. Lakini mashirika mangapi ya Serikali na taasisi za umma zinadaiwa bili kubwa ya umeme, tuanze kukamata huko. Wananchi walio wengi hawawezi kubeba deni hili zito. Tukiangalia deni hili ni kubwa lakini leo tuanze kuwapelekea wananchi waanze kulilipa, hicho hakitokwenda sawa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi nimeshatoa ushauri na ninaona hoja hii kuna umuhimu sana wa kuijadili leo japo si kwa dakika nyingi kama tunavyofanya, lakini kwa maslahi ya wananchi wetu. Wananchi walio wengi sana wameanza kuathirika hata vipato vyao lakini hata familia zao. Wengine walikuwa walipe madeni ya watoto maskuli wameshindwa wanalipia umeme. Umeme ukitia shilingi elfu thalathini (30,000) basi siku mbili umekwisha. Mwananchi gani wa kawaida hata wale wengine wanaoweza ku-*afford*.

Lakini labda tuambiwe tu wafanyakazi wa Shirika la Umeme wanapewa *units* ngapi kwa mwezi na tujumuishe, *units* zile wanazopewa ni kiasi gani Shirika linakosa mapato.

Mhe. Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha sana na tunasema hili kwa uchungu mkubwa sana, kwa sababu wananchi walio wengi sasa hivi wameathirika maisha yao kutokana na pandisho hili la umeme.

Mhe. Naibu Spika, lakini hoja imesema Kifungu cha 36 kuwa ndiyo Kifungu ambacho *ZURA* ilitakiwa itoe *public hearing* ili wananchi watoe maoni yao juu ya kupandishwa kwa umeme. Lakini jambo hili halikufanywa, na kama jambo hili halikufanywa sheria hii iliyompa mamlaka Waziri kutangaza ni batili.

Sasa tunaomba sana Serikali kupitia hoja hii, Serikali kupitia Wawakilishi wa wananchi wa majimbo na waliokuwa siyo wa majimbo, ifute mara moja amri yake ya kuweza kuzidisha umeme na kurudi kwenye mstari, tuone tukachukue basi maoni ya wananchi ili tuone wananchi wametoa maoni gani. Lakini

tukifika pahala rafiki yangu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Zanzibar, Mwanasheria msomi, alisema tunaweza kuvunja utaratibu.

Lakini ninataka kumwambia utaratibu huu umeanza kuvunjwa na Serikali. Sasa ukiwa umevunjwa na Serikali na sisi tuendelee? Sisi hatuendelei, wala hatutaki kuvunja sheria, lakini tumeleta kukumbushana. Kila mtu kwa imani yake na kila mtu anajua, waislamu wakati wa sala ukifika adhana ndiyo inasomwa ili kuwa na ukumbusho. Kwa hivyo sisi leo tunaikumbusha. Ninataka nimwambie tu Mwanasheria Mkuu tulia tutakukumbusha kadri ya hali hii itakavyowezekana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana na naunga mkono hoja hii asilimia mia. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mohammed Said Mohammed. Mchangiaji wetu wa mwisho katika upande wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi atakuwa ni Mhe. Simai Mohamed Said, karibu.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi naomba kwa ruhusa yako niweze kwanza kumpongeza Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Paje Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa kuja na hili wazo na hoja. Na nitapenda niende moja kwa moja kwenye hoja ili niweze kuchangia hii hoja.

Mhe. Naibu Spika, kwenye Sura ya Pili ya Katiba ya Zanzibar Kifungu Nam. 10 kinasema hivi,

"Kwa madhumuni ya kuendeleza umoja na maendeleo ya watu na ustawi wa jamii katika nchi, itakuwa ni wajibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar:-

> (a) Kutoa huduma za kutosha kwa ajili ya kuendeleza watu katika njia za mtu kuwa huru kwenda atakapo na utoaji wa huduma kwa watu wote na kutoa haki zote za kuishi kwa Mzanzibari sehemu zote za Zanzibar.
>
> (b) Kuondosha kabisa vitendo vya rushwa na utumiaji mbaya wa cheo dhidi ya umma kwa wale wote walio na madaraka".

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha karibuni nilikuwa ninapokea simu na *messages* za vitu viwili kwa Wazanzibari wanaoishi katika jimbo langu, Wazanzibari wanaoishi hapa mjini na Wazanzibari wa maeneo tofauti.

Matamko mawili yaliyotoka. Moja ni la upandishaji wa bei juu ya nishati ya umeme na la pili ni suala la ardhi.

Lakini hapa nitachangia kwenye suala la umeme ndiyo hoja iliyopo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, tulipokuwa tunasoma maskulini zamani kwenye darasa la tatu, la nne, unaambiwa *the basic needs of human being*; *food, shelter* yaani pahala la kupumzikia na kuweza kulala na mavazi (*clothing*).

Kwa hivyo ninataka niseme, kwanza itambulike kwamba suala la umeme siyo kitu ambacho ni *luxurious* ambacho mtu anachotaka kustarehe nacho. Ni kitu cha lazima kwa kila Mzanzibari. Na nchi yetu ni nchi ambayo tunatawala kwa msingi wa demokrasia.

Na ukiangalia katika hotuba ya Rais alipokuja hapa Barazani kwenye ukurasa wa 47, alizungumza,

"Aidha Shirika la Umeme la Zanzibar (*ZECO*) litafanyiwa mabadiliko ili liweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi na kujiendesha kibiashara".

Mimi ninaunga mkono mawazo haya lakini utaratibu uliotumika naona kama hapa siyo sahihi. Ikiwa Sheria inataka hicho Kitengo cha *ZURA* kufanya hiyo *public hearing* ambayo Wajumbe wengi ndani ya Baraza hili na wananchi walipatwa na mshituko baada ya hilo tangazo lilipotoka katika mwezi huo uliopita.

Sasa ninataka niseme kwamba kwa haya ambayo yaliyozungumzwa, tunataka tutambue nchi yetu bado wananchi wetu ni maskini. Na naomba nichukue hichi kitabu, ninataka ninukuu kidogo Sura ya Sita, Kitabu cha Kuli cha Adam Shafi.

"Ilikuwa ni asubuhi na mapema, upepo mkali unavuma, wavuvi walikuwa wanarejea kutoka baharini na kutokana na dhoruba ya usiku iliyopita walikuwa hawakupata hata samaki mmoja. Kwa upande wa machomozo ya jua, mawingu ya manjano yalichanganika na mawingu ya kibluu na kuipamba mbingu yote. Rashid alikuwa amesimama kando ya pwani ya Gulioni, pote palijaa milio ya kunguru waliokuwa wakiruka kutoka mikokoni kwa mia kuelekea majumbani katika kutafuta rizki.

Kwa mbali kutoka pale aliposimama Rashid aliweza kuziona meli zilizokuwa zimetinga nanga. Alisimama hapo na kufikiri kazi ya siku ile ya kwenda kuingia ndani ya mameli yale na dhoruba kama ile. Kazi ya ukuli ilikuwa ni

ngumu iliyomchosha kabisa Rashid, lakini alikuwa hana la kufanya ila kuendeleza nayo ili aweze kupata maisha. Pesa zenyewe zilikuwa hazitoshi, matumizi yake yanazidi na madeni yanapotea. Mbali ya kidani cha mama yake alichoweka rehani alikuwa anadaiwa na washiriki chungu nzima kwenye maduka".

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema awali nchi yetu ni maskini, watu wetu ni maskini. Hata sisi binadamu ukitaka kufanya jambo lolote kuanza kula, unakula chakula cha kianzio kinaitwa *starter*, unakula chakula kikuu ambayo ni *main course*, halafu unakula cha *dessert* ambacho ni chakula kitamu. Wananchi wamelishwa moja kwa moja vyote, hivi ndivyo binadamu unaweza ukaingiza supu, samaki huku na kati kati ukatia keki ukala kwa pamoja, haiwezekani, lazima twende kwa utaratibu. Lazima mwananchi ajipange, asilimia 20 ni tozo kubwa. Hata hawa wawekezaji katika sekta ya utalii ambao mimi ni mdau, wanapanga mambo yao miezi kumi na mbili kabla.

Leo utakapopandisha asilimia 20 tunaharibu mfumo mzima wa maisha ya wananchi wetu, wananchi wetu wanaotupa kodi, wawekezaji. Kazi ambazo Waziri wetu wa Fedha anahangaika kuleta wawekezaji lakini mipango inayopangwa inakuwa haiendi vilivyo.

Nilikuwa ninasoma hotuba nyengine hapa ya Rais wa Marekani Jimmy Carter. Kwenye hotuba yake ya mwaka 1977 kuna kifungu ninanukuu hichi, alisema;

"The world itself is now dominated by a new spirit. People more numerous and more politically aware are craving, and now demanding, their place in the sun-not just for the benefit of their own physical condition, but for basic human rights".

Mhe. Naibu Spika, mwananchi sasa hivi anapokaa anapotaka kujipanga mahitajio yake anayajua, na Serikali hii mwaka mmoja nyuma hapa tulikwenda kwa wananchi tukawaomba na tukawaahidi nini tutawafanyia ili maisha yao yawe bora. Hili tunalolifanya sasa hivi ni kwenda kinyume na yale ambayo tuliyoahidi hasa kwa Chama cha Mapinduzi ambacho kipo madarakani na ni chama tawala. (*Makofi*)

Na mfumo huu kama tutaendelea tutakapofika mwaka 2020 wananchi wetu hawatotufahamu. Mimi ninachokiomba binadamu tumeumbwa na Mwenyezi Mungu sisi, lakini siri kubwa aliyotupa Mwenyezi Mungu ni kusahau. Leo tulipo hili je, tumewasahau wananchi kwa haraka sana kiasi hicho. Leo unamwambia mtu ambaye anapokea shilingi elfu kumi kwa siku, elfu mbili

peke yake iende zake kwenye kulipia umeme. Na kwenye umeme huo utakaponunua kuna *tax and infrastructure*, kuna *VAT* na mengineyo.

Sasa mimi ninachoomba Mhe. Naibu Spika, kwa suala hili nimemsikia Mhe. Mwanasheria Mkuu amesema kwamba kwa mujibu wa sheria hii hawa wananchi wanatakiwa wao moja kwa moja waende katika Mahakama, na kuna vifungu ambavyo vimewekwa vya kisheria. Lakini aliyetangaza ni Waziri, na huyu mwananchi atakwenda kwa nani. Kwa hivyo mwananchi moja kwa moja ataangukia kwetu sisi Wawakilishi kuja kuleta manung'uniko yake, na sisi tukiwa ni Wawakilishi wa wananchi na kazi yetu ni hii. Basi mimi naomba Serikali yetu ni sikivu, Rais wetu wa Zanzibar Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein ni mtu muungwana, mwenye busara na Serikali yake pamoja na Mhe. Makamu wa Pili. (*Makofi*)

Ikiwa Waziri ameteleza ni kawaida ya binadamu, hakuna binadamu aliyekamilika. Asimame mbele yetu atueleze, na kama anaweza kulifuta wananchi hawawezi kumuhukumu watafurahi, kitendo ambacho atakachokifanya.

Mimi ninachokiomba hili suala la asilimia 20 arudi tena kwa wananchi, kama Sheria inavyomtaka ili wananchi waweze kutoa mawazo yao...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa malizia dakika moja.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo ninachokiomba Serikali yetu ni sikivu kama nilivyosema. Ninachokiomba sana Mhe. Waziri kwa hoja ambayo ameileta Mhe. Jaku Hashim Ayoub ambaye kwa kweli ni Mwakilishi mmoja ambaye ni mzoefu, mawazo yake ni kwenda kuisaidia Serikali na kuishauri, ametimiza wajibu wake. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mimi ninamuomba sana Mhe. Waziri atupe sisi na hizo sifa ambazo Serikali yetu huko mbele turudi tena kwa wananchi pande zote mbili; Serikali na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao ni washauri hapa kwa mujibu wa Katiba, ili twende vifua mbele kwa wananchi, ili kwamba mawazo yao, fikra zao na manung'uniko yao yamesikika na ili haya tuweze kwenda kwa pamoja. (*Makofi*)

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub na wale wote waliochangia hoja hii. Nikushukuru pia wewe Mhe. Naibu Spika, kwa busara zako unazoendelea kutuongoza hapa.

Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Simai. Waheshimiwa Wajumbe sasa nitampa nafasi pia Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Hamza Hassan Juma ana mchango na yeye wa kuchangia na baada ya hapo kwa upande wa Serikali atakuja Naibu Waziri wa Ardhi ambaye na yeye kidogo atatoa majawabu lakini vile vile nitampisha na mwenyewe mwenye Wizara hii Mhe. Salama Aboud atachangia, na baadae Mhe. Mohammed Aboud Mohammed ambaye ni Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili ambaye yeye atachangia na atazungumza kwa niaba ya Serikali.

Kwa hivyo nimpishe sasa hivi Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Hamza, ninakupa muda kama wa dakika tano, ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, na mimi ninataka nikushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia machache katika hoja hii mahususi aliyoleta Mheshimiwa makini kabisa Mhe. Jaku Hashim Ayoub, ambaye ni Mwakilishi wa Jimbo la Paje. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza nataka nianze kwenye Katiba. Katiba yetu ya Zanzibar Ibara ya 43 (5), naomba niinukuu inasema:-

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Mamlaka ya Rais ndiyo itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi ya juu ya Sera za Serikali kwa ujumla na Mawaziri chini ya uongozi wa Makamu wa Pili wa Rais watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar".

Mhe. Naibu Spika, vile vile nitaomba ninukuu Ibara ya 88 (d) ya Katiba yetu ya Zanzibar ambayo inasema:-

Moja katika majukumu ya Baraza la Wawakilishi ni kuidhinisha na kuisimamia mipango ya maendeleo ya Serikali katika njia ile ile ambayo bajeti ya mwaka inaidhinishwa.

Mhe. Naibu Spika, nimetaka nianze na haya ili kuonesha umuhimu wa kazi yetu na majukumu kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika kuisimamia vyema Serikali yetu ili iweze kufanya kwa mujibu wa Katiba na sheria ambazo tumezitunga.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwanasheria Mkuu aliposimama alitueleza tujitahidi sana Baraza hili lisije likakiuka ile misingi iliyojiwekea yenyewe. Sheria zote za Zanzibar pamoja na Katiba ya Zanzibar zimetungwa na Baraza la Wawakilishi. Sasa katika suala hili ninadhani ni vyema sote, kwa sababu Wawakilishi *backbenchers* pamoja na Mawaziri wote ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, ninadhani wasia ule uwe katika pande zote mbili, kwamba sote tujitahidi tufuate sheria zetu tusije tukakiuka ile misingi ambayo tuliyoiweka. (*Makofi*).

Sasa ninakuja katika hoja. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kama alivyosema Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba mamlaka ya kutangaza bei ya umeme kwa mujibu wa Sheria tuliyoitunga, tumeipa taasisi ambayo ipo chini ya Kamati yangu ambayo ipo Wizara hii hii ya Maji, Ardhi na Nishati.

Sasa mimi nadhani Mhe. Naibu Spika, Serikali naiomba nikiwa mimi kama Mwenyekiti wa Kamati, ili tusisokotane sana na Wajumbe kwa hoja ambayo ipo kisheria zaidi. Mimi ninadhani kama Serikali itakuwa imeteleza kidogo katika hili, mimi ninadhani suala la kusema kuomba radhi lakini vile vile turudi katika ule msingi ambao uliokuwa upo sahihi. (*Makofi*)

Vile vile kama tutafanya hivyo tutavipa heshima na nguvu zile mamlaka ambazo tumezipa madaraka kwa kusimamia yale majukumu. Lakini hili Mhe. Naibu Spika, ninataka nilizungumze katika njia mbili. Mimi Mhe. Waziri ninataka nimtetee kwa ugeni wake au kwa upeo wake katika wizara hii na suala la umeme Mhe. Naibu Spika, mimi nikiwa Mwenyekiti wa Kamati tumelizungumza sana suala la deni la Shirika la Umeme la Zanzibar hasa kutoka *TANESCO*. Mzigo tunaowabebesha Shirika la Umeme Mhe. Naibu Spika, ni mzigo mkubwa sana.

Shirika la Umeme linanunua umeme kutoka *TANESCO* bei ya juu kuliko ambayo inayowauzia wananchi. Lakini leo.

Mhe. Waziri amechukua hii nafasi, pengine inawezekana aliwasiliana na watu wake, labda taratibu nyengine watakuja kueleza hapo baadae. Kitu ambacho ninakiona ni kwamba sisi wenyewe ambao tunapitisha hii bajeti, na suala hili namuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alisimamie sana. Nilitegemea Mhe. Waziri wa Fedha angekuwepo hapa, suala hili nadhani kama litaweza kutekelezwa, mimi nadhani isingefikia pahala kukatokezea mtafaruku kama huu tulionao sasa hivi.

Leo katika taasisi ambazo zinadaiwa fedha nyingi sana na Shirika la Umeme ni taasisi za Serikali. Mhe. Naibu Spika, sisi kila mwaka tunapitisha bajeti, na bajeti tunapopitisha hatupitishi *lump sum* kama bajeti nzima ya wizara, tunapitisha idara kwa idara na kifungu kwa kifungu. Sasa leo Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa una dakika moja ya kumalizia.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, leo kama ingekuwa wizara za serikali zinalipa madeni yake vizuri. Mimi nafikiri kadhia hii isingefikia kuwa hapa. Lakini kuna *ZRB* ambapo sasa hivi wamekuwa kama wana mafuta kidogo, wanadaiwa na Shirika la Umeme karibu bilioni 6, sio milioni 6, bilioni 6. Leo taasisi hizi bado zinaendelea na mazungumzo sijui na nini, na kwa sababu sheria ambayo *ZRB* tuliyoitungia hapa, yeye ndio anatakiwa akubali lile deni. Mpaka leo wanawapiga danadana huku na huku, lakini Shirika la Umeme linakusanya fedha kila mwezi, na fedha zile zinakwenda katika mfuko mkuu wa serikali. Wao wanatakiwa wapelekewe *returns* zao karibu milioni 300 kwa mwezi, ili kuweza kufanya shughuli zao za kusambaza umeme vijijini, fedha zile hawazipati Mhe. Mwenyekiti, sasa watafanya nini, ndio kama hivyo. Inapokuwa sasa kapu haijai, inabidi sasa unaanza kuingia mtaani unakamata kamata mpaka vipaka vidogo vidogo.

Sasa serikali ili kadhia hii na Mhe. Waziri wangu tusimtie kwenye matatizo, serikali tuangalie katika bajeti zile fedha tulizozitenga kwa ajili ya kulipa Shirika la Umeme walipe. Vyenginevyo Mhe. Naibu Spika, kila siku Shirika la Umeme litakuja litatupandishia, lakini kwa kweli kama hatuwezi kuwalipa watafika pahala wata- *collapse*.

La mwisho kabisa kwa kumalizia. Mhe. Naibu Spika, mimi naomba, kwa sababu hili Shirika la Umeme limekuwa ni shirika la serikali, lakini imekuwa kama ni idara ya serikali, kwa sababu linaendeshwa kwa kufuata maagizo ya serikali ili wananchi waweze kupata afueni. Sasa hili mimi nafikiri Mhe. Naibu Spika, kama serikali na mawaziri wote wako hapa, kama wataangalia katika *OC* zao wakaweza kulipa vizuri *bill* ya umeme, mimi nafikiri matatizo haya hayatoweza kuja kujitokeza.

Sasa suala la wananchi kwenda kulalamika kule kwa *ZURA*. Mimi nafikiri *ZURA* jambo lolote watakalolifanya wao, akipelekewa malalamiko wataweza kuyatatua. Lakini jambo ambalo hawakulifanya wao nadhani Mhe. Mwanasheria Mkuu hili litabakia kuwa hivyo. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa ya kuchangia kwenye hoja hii ambayo imeletwa mbele yetu. Ni kweli kwamba bei ya umeme imepanda kwa karibu asilimia 20. Lakini tunapaswa kujua ni kwa sababu gani, hii inatokana na gharama za kuendesha hizi shughuli.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo tukumbuke na hatuna haja ya kutisha watu, kwamba mpaka sasa wananchi wanaoishi Zanzibar licha ya kwamba kuna pandisho la asilimia 20 wanalipa nafuu kuliko kule ambako unatolewa Tanzania Bara. Kwanza naomba tufahamu hivyo. Sasa kama leo tunalia kwa sababu tu asilimia 20 imepanda, lakini bado tunalipa chini kuliko wale kule ambako tunautoa, siku moja ikifika tukawa tunalipa sawa sawa sisi na wale Bara tutasemaje na tukizingatia kwamba sisi mpaka sasa hatuna chanzo chetu hapa. Sahihi ni lipi? Mnataka Shirika lishindwe kujiendesha ili yasemwe mengine zaidi, ama tunataka unafuu wa watu wetu.

Mhe. Naibu Spika, manung'uniko hayamaliziki, kwa sababu hata tutakalolifanya kuna mwengine atalitafsiri vyengine. Lakini tuseme kwamba serikali kwa nia thabiti imejitahidi kubeba mzigo mkubwa kufanya unafuu kwa wananchi wake, ushahidi tosha ni huo. Lakini inaonekana hapa kuna shida kidogo ya tafsiri ya sheria.

Mhe. Mwanasheria kasema vizuri sana, kama kuna mtu kahisi kwamba labda kuna utaratibu ulikosekana, basi namna ya kuharakisha au kufanya kufanywe vizuri njia bora kazitaja ambazo ni za kisheria zaidi.

Mhe. Naibu Spika, lakini tukumbuke kwamba hata leo hii kutokana na ule ukosefu wa kutafsiri sheria vilivyo, mnakumbuka hapa kati maneno mengi yalikuwa na wengi ama wote kati yetu tunasema sio halali kwa sababu tu ya ukosefu wa kutambua sheria. Watu wanapiga kelele mpaka kesho eee, kwa sababu sheria hawakufahamu vizuri, tusiwe kama hao. Sasa mimi naomba ushauri. Kwa mujibu wa Katiba kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Hamza Hassan, kifungu cha 88(c) moja kati ya kazi za Baraza la Wawakilishi ni kuuliza, basi ningeomba ingekuja katika mfumo wa swali kuliko kwanza kuwatisha watu.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana, na mimi siungi mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri nakushukuru. Sasa tutampisha Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Karibu Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe, mimi naomba kuchangia kujibu hoja iliyotolewa na Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Paje Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kuhusu utaratibu na kutangaza kwangu kwa bei ya umeme.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kulijulisha Baraza lako tukufu, lakini vile vile kuwajulisha wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla kuhusu utaratibu wa kupandisha bei ya umeme umefuata sheria, taratibu zote, miongozo yote na hatimaye leo ndio maana nikaweza mimi kama Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kusimama na kuweza kutoa tangazo, ambapo ndani ya tangazo langu kama watu wamenisikiliza kwa makini nilizungumza nia na dhamira ya serikali. Dhamira ya serikali ni kuhakikisha kwamba wananchi wake wakati wote wanaishi kwa amani na utulivu, lakini wananchi hawa wanaweza kupata huduma ambayo ni lazima kwa bei rahisi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, pia niliweza kutoa historia ya jambo lenyewe katika tangazo, nikasema historia *ZECO* waliomba miaka miwili nyuma, kuomba kupandishiwa bei ya umeme baada ya wenzetu Tanzania Bara kutupandishia umeme. Lakini kwa dhamira ile ile na nia nzuri ya serikali, ikawa inaangalia mambo mengine ya msingi na mambo muhimu, lakini hatimaye serikali ikaweza kufanya maamuzi mwezi Agosti 2016. Kwa hivyo, serikali baada ya kufanya maamuzi serikali hiyo hiyo ilichukua jukumu la kufuata utaratibu na sheria ambazo imeziweka, hakuna sheria ambayo imevunjwa, *ZURA* pamoja na *ZECO* kwa kushirikiana baada ya bodi zote mbili kukaa pamoja, kwa sababu walikaa pamoja wakajadiliana, *management* ya *ZECO* na *management* ya *ZURA* walikaa pamoja walijadiliana na wakakubaliana, wakafanya vitu vyote kwa kuridhia kupandishwa kwa bei kwa asilimia 20.

Lakini utamaduni uliofanyika pia wa kutoa elimu kupitia Redio Zanzibar na kupitia *ZBC*, na wananchi wakichangia. Kazi ilifanywa kwa muda wa miezi miwili nilitakiwa nitangaze umeme ule Agosti 2016, lakini sikuweza kutangaza kwa sababu ya hayo hayo kwamba Redio na *ZBC* ilikuwa bado vipindi vile havijatolewa. Lakini vipindi vikatolewa mfululizo na nilimuomba mwenzangu hapa kunipunguzia gharama, na kazi ilifanyika na wananchi wakatoa hoja zao na ilikwenda kwa utaratibu mzuri.

Mhe. Naibu Spika, baada ya elimu ile, kwa sababu ile ilitakiwa kuanzia Novemba 1 iweze kutumika, hapo ndipo nilipotoka. Lakini katika umuhimu wake na kwa uzito wa jambo lenyewe, kwa umuhimu wake Mhe. Naibu Spika, na Waheshimiwa Wajumbe na kwa uzito wa jambo lenyewe, hatuwezi kulinganisha kupandishwa kwa bei ya umeme kwa wakati huu na kupandishwa kwa mafuta ambayo imelinganishwa na mtoa hoja, ambapo bei ya mafuta, gesi na mafuta ya taa tunapandisha kila mwezi, na mimi ndio ninatoa ruhusa baada ya kukaa *ZURA* wakinileta kwamba sasa hivi itangazeni. Lakini kwa umuhimu wake tukakubaliana, tukasema hili lina umuhimu na waziri mwenyewe mwenye dhamana, mwenye mamlaka ya *ZECO*, lakini mwenye mamlaka ya *ZURA* ambayo iko chini ya wizara yangu, kwamba waziri tungekuomba ulifanye hili jambo wewe mwenyewe.

Kwa sababu ya nia nzuri ya serikali na uzito wa jambo lenyewe, basi nikalifanya jambo hilo bila ya kimeme, bila ya wasi wasi na kuwaeleza dhamira ya serikali, kwa sababu dhamira ya serikali kama nilivyosema mwanzo ni kutoa huduma bora kwa wananchi wake, lakini kuwafanya wananchi wake hasa wenye kipato cha chini kuweza kukidhi mahitaji ya lazima. Ndio maana katika maelezo yangu niliyotoa nilisema kwa kina kwamba bei ya umeme ukilinganisha kutoka Tanzania Bara na bei ya umeme ambayo Zanzibar tunanunulia ni bei mbili tofauti. Zanzibar tunanunua umeme kwa bei nafuu, kwa sababu serikali inawahurumia wananchi wake wenye kipato cha chini.

Mhe. Naibu Spika, nawaambia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi kwa jumla, dhamira ya serikali inawapenda wananchi wake sana, na ndio maana mzigo mzito serikali imeamua kuubeba. Serikali kwa kupitia kwa Dk. Ali Mohamed Shein, kwa dhamira kabisa ndani ya nafsi yake akasema huu mzigo basi tuwapunguzie wananchi wetu, lakini jukumu hili Mhe. Waziri tunaomba ulichukue. Kwa hivyo, mimi naomba niseme na wananchi wafahamu kabisa kwamba serikali hii ina nia safi na wao, inawapenda na inawathamini na ndio maana tukafika hapa tulipofika. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naomba niseme wazi kwamba hakuna utaratibu wowote wa kisheria uliovunjwa, wala hakuna nia mbaya yoyote serikali iliyokusudia kwa watu wake, serikali itaendelea kuwa na dhamira na nia safi kwa watu wake, chini ya jemedari Dk. Ali Mohamed Shein, na sisi wasaidizi wake tuko tayari kufuata nyayo zake, hatutokwenda kinyume na utaratibu. Naomba niwathibitishie kwamba, tunafanya kazi wakati wote kwa mashirikiano, tunafanya kazi kwa kujiamini na tunafanya kazi kwa kuangalia sheria zote zinazohusika.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba katika suala hili wananchi wengi wa Zanzibar wametupongeza sana, na hata wenzetu wa Tanzania Bara, kwamba tumeona thamani ya kuwapunguzia umeme, tumepata pongezi nyingi sana kwa jinsi tulivyoona thamani ya kuwapunguzia umeme wananchi wa Zanzibar na kwa kuwauzia umeme kwa bei nafuu zaidi.

Naomba kuwasilisha, siungi mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri kwa majibu yako mazuri sana. Sasa mwisho kabisa nitampa nafasi kabla ya kumpa mtoaji hoja, nitampa nafasi Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambaye atatoa kauli ya serikali, baada ya hapo nitampa nafasi aliyetoa hoja na yeye kueleza machache. Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi.

Pia nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri na Naibu wake kwa maelezo mazuri waliyoyatoa kwa niaba ya serikali.

Pia niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuwa makini wakati wote kuona namna ya kuwasemea wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, nataka niseme kuhusu imani ya serikali kwa wananchi wake, kama alivyosema Mhe. Waziri anayehusika na wizara hii, iko kwa hali ya juu sana. Nia na dhamira ya serikali ni kuhakikisha bado umeme unapatikana kwa wananchi wote na shirika lenyewe liweze kujiendesha, kutoa huduma bora na nzuri kwa maslahi ya wananchi na maslahi ya taifa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo kupandishwa huko kwa bei ni uamuzi wa serikali, ili kuhakikisha kwamba bado wananchi wetu waendelee kupata umeme na bado tuhakikishe Shirika letu la *ZECO* linafanya wajibu wake. Vyenginevyo shirika linaweza kushindwa kufanya kazi zake na matokeo yake yakawa magumu zaidi ya kukosa umeme sote.

Kwa hivyo, maamuzi yale tunaelewa yana ugumu kwa wananchi wetu kwa kiasi fulani, lakini yatakuwa magumu zaidi kwa kutoyatekeleza yale kwa kukosa kabisa umeme wenyewe. Kwa hivyo, kwa kiasi kikubwa sana serikali bado inachukua nafasi kubwa ya kufidia sehemu hiyo ya umeme, ili tuendelee kupata umeme. Ingekuwa kama alivyosema Mhe. Waziri muda mrefu ilikuwa matangazo ya kuongeza bei ya umeme yatoke, lakini kwa imani hii ya serikali

ilifanya kila jitihada kuvuta wakati na kutafuta kila aina ya kuziba pengo ili huduma hiyo iweze kuendelea.

Mhe. Naibu Spika, mimi naamini kwamba Wajumbe wa Baraza hili tukufu na wananchi kwa jumla, wataona jitihada kubwa zinazofanywa na Shirika letu la Umeme la Zanzibar. Sasa hivi kwa kiasi kikubwa sana mijini na vijijini tunapata umeme tena kwa uhakika zaidi. Kilichotokea, *ZURA* ni taasisi ya serikali, waziri ni wa serikali, anapotangaza kwa niaba ya chombo chake, kwa maana ya *ZURA*, alifanya hivyo kama nilivyoeleza baada ya kukutana na bodi zote mbili wakakubaliana kwa uzito wa jambo lenyewe alitangaze Mhe. Waziri. *(Makofi)*

Kwa hivyo, sasa alifanya hivyo kwa dhamira njema. Kwa hivyo, dhamira yake njema hiyo tusiitafutie kasoro. Kwa sababu upo utaratibu mzuri tu uliowekwa na sheria yenyewe, Mhe. Mwanasheria Mkuu alieleza. Kwa hivyo, kama kuna kosa au hakuna kosa chombo cha kuamua kipo kwa mujibu wa sheria, na kwa bahati nzuri sheria hiyo kifungu cha 38 cha *ZURA* kilieleza vizuri sana namna ambavyo inapotokea wananchi kutokuridhika na bei inayotangazwa ili kupeleka malalamiko yao.

Kwanza inaanza kwa mamlaka yenyewe, kama maamuzi ya Mamlaka hayakuwaridhisha basi wanayo haki ya kwenda kwenye bodi, na kama maamuzi ya bodi hawakuridhika nayo kifungu 38.6 ya sheria hii, inaeleza kwenda mahakamani.

Kwa hivyo, utaratibu mzuri umewekwa na alivyofanya Mhe. Mwanasheria Mkuualitutaka Baraza hili tusiende nje ya utaratibu wa sheria tulizozitunga sisi wenyewe, alituelekeza vizuri, bado sisi kwa pamoja tusije tukavunja hiyo sheria sasa ya kujichukulia mamlaka ambayo tayari tumeyatoa yatekelezwe na vyombo husika.

Kwa hivyo bado Waheshimiwa Wajumbe jambo zuri katika eneo hili tuiachie sheria ichukue mkondo wake. Malalamiko yaliyopo yapelekwe kwenye hivyo vyombo vilivyotajwa ili sote kwa pamoja humu tusije tukaonekana Baraza lenyewe sasa linavunja sheria wananchi wetu hawatotuelewa, chombo hichi ni kikubwa sana, heshima yake kubwa katika nchi lazima heshima hiyo iendelee kuwepo na iheshimiwe na sote. Sasa ikiwa sisi watunga sheria tunataka kuanza utaratibu wa kuivunja sheria yenyewe kidogo napo kueleweka kwetu kutakuwa kugumu, na anapokosea mtu sheria wewe mwengine hutakiwi ukosee zaidi, unatakiwa wewe urekebishe.

Kuna maneno yanayosema " Kutokujua Sheria si kusameheka kwenye sheria yenyewe" kwa hivyo chombo chetu hichi kwa nia njema kabisa tungekubaliana na ushauri ambao Mhe. Mwanasheria Mkuu ameutoa kwa wananchi kupeleka malalamiko kama wameona bei ni kubwa, lakini tuelewe tutakapopeleka malalamiko hayo na *ZECO* wakashindwa kutoa huduma, maana yake nchi yetu itakuwa kiza, tunafanya vile jamani tukubaliane tunataka maendeleo ya nchi yetu na lazima sote tubadilike tuijenge nchi hii, tuwe *committed* kwa kufanya mambo ya msingi yatakayoleta mabadiliko twende mbele.

Katika eneo moja ambalo linaleta mabadiliko makubwa ya kimaendeleo ni umeme. Jana nilikuwa natazama Televisheni walionesha kijiji kimoja Singida huko kilivyokuwa hakina umeme kabla, na baada ya kupata umeme mambo yalivyokuwa na unafuu zaidi yakifanyika na shughuli za maendeleo zilivyokuwa. Kwa hivyo katika dunia ya leo Serikali yetu inaangalia *source* nyengine za kupata umeme wa unafuu, si kwamba hii shughuli ya kupata umeme kwa njia moja tu ya kutokea upande wa Tanzania Bara, lakini bado huku ndani kuna *study* nyingi zimefanywa na mipango mingi inawekwa ili kuona njia nyengine za namna ya kupata umeme kwa njia nafuu. Kazi hiyo inafanywa na Serikali kwa nia ya kuwahurumia wananchi wetu, kwa nia ya kujua kwamba maendeleo yetu yanahitaji umeme.

Kwa hivyo mimi niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukubaliane tuondoke hapa kwamba tuiachie sheria hii ichukue mkondo wake kama maelekezo aliyotoa Mwanasheria Mkuu, na mimi naridhika sana na maelezo ya Waziri, na bado hoja hii tuiache tusiiunge mkono ili tufanye mambo kwa mujibu wa sheria na sote tusiwe wakosaji wa sheria.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Sasa nampa nafasi Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa dakika tano, naamini kwamba dakika tano zinatosha. Karibu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, hii hoja kwenye dakika tano nitakuwa sijawatendea haki wananchi wa Unguja na Pemba kwa kujibu hoja za Mawaziri, dakika tano ni kidogo, hoja ni nzito. Naomba tutumie kanuni ya kuweka muda wako kando sijui kanuni ya ngapi ile, lakini kwa dakika tano nitakuwa sijajibu kitu, watu hawa wanane kwa kila mmoja kunipa dakika moja itakuwa sijafanya haki. Mhe. Naibu Spika, nahitaji muongozo wako zaidi.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa kwani wewe unajibu yote ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Mawaziri au unatoa maelezo yako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Najibu hoja za Mhe. Waziri ili wapate kufahamu. Unajua Mhe. Naibu Spika, mtu ukitaka kumfahamisha biashara faida yake …

Mhe. Naibu Spika: Mimi nafikiria nitakuongeza dakika nyengine tatu naamini kwamba utamaliza, kwa hivyo nakupa dakika saba.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ukinipa hata kumi sio mbaya Mhe. Naibu Spika, hili jambo ni muhimu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nimtoe wasi wasi *AG*, *AG* kuna hadithi ndogo tu kuna simba siku moja alilala alishiba sana akaja akapita panya akamruka, akamwambia unanikera mbona hata sikio langu kubwa kuliko panya wewe, akamwambia niachie kuna siku nitakusaidia, akamwambia katika maisha yako hutanisaidia, akamkamata akamrembea huko. Sasa kuna siku yule simba akanasa kwenye nyavu, panya yule yule akaja akamsaidia akakata kamba akamwambia ile siku ndio leo.

Sasa *AG* usiogope aibu kwa kukoselewa na Jaku, mimi si msomi, mimi sikusoma ndio maana ukaona sijapata Naibu Waziri au Waziri usiogope kukoselewa na Jaku kabisa, katika majumuisho naomba unioneshe Sheria ya Haki, Kinga na Fursa za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kifungu cha 49 Mhe. *AG* naomba usikilize kidogo kwa makini.

Kifungu cha 49 ambacho kinanipa mamlaka ya Baraza na kamati kutumia vikao vyake katika kuleta haki ya maslahi ya wananchi, hivyo basi hoja hii huwezi kukataa Mhe. *AG*. Mnajua makosa mnafanya nyinyi Waheshimiwa Mawaziri, mkishakukaa kule BLM msiogope kukosolewa na Jaku, Waheshimiwa Mawaziri hakuna mkamilifu, ndio hadithi niliyokutolea. Mkishakukaa nyinyi mnaona kama si aibu …

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku hii hoja haikukataliwa Mheshimiwa alisema kutokana na maoni yake kwamba hatuwezi kuvunja sheria ndio alichokisema, na mimi hoja nimeiachia imeendelea. Kwa hivyo huna sababu hapa tena ya kuanza kuzungumza vitu ambavyo tayari tumeshavimaliza, endelea na hoja yako mambo mengine lakini sio kauli ambayo amesema Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza hoja haikatazi hapa kanuni katika kuleta hoja, kuna sheria ya Kinga, Haki na Fursa za Wajumbe kifungu cha 49 Mhe. Naibu Spika, ambacho kinanipa mamlaka ya Baraza na Kamati kutumia vikao vyake katika kuleta haki na maslahi ya

wananchi, hivyo kuleta hapa sio kosa, itambulikane kuwa si kosa kufanya hivi kisheria, ni wajibu wangu na kwa mujibu wa sheria.

Kwanza nichukue fursa hii kuwashukuru wote waliochangia hoja hii na kuna wengine sijui uliwapa au bahati mbaya hii hoja ilikuwa na watu wengi au muda haukutosha, nitambue kuwa mchango wa bosi wangu Mhe. Ali Suleiman Ali *(*Shihata*)*, Mhe. Abdalla Ali Kombo niutambue huo mchango wao, hapo kwa maandishi na *hansard* zikae sawa.

Mhe. Naibu Spika, waliochangia hoja hii ni watu wanane au Waheshimiwa wanane niwatambue kwanza kwa kuwataja haraka haraka.

1) Mhe. Abdalla Maulid Diwani
2) Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
3) Mhe. Makini na mtaalamu wa Sheria Mhe. Mohammed Said nimpongeze
4) Mhe. Simai Mohamed Said
5) Mhe. Hamza Hassan Juma
6) Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji na Nishati
7) Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji na Nishati (msomi)
8) Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais (mtetezi wa Mawaziri).

Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwa ufupi hoja ameikubali na ameiona. Nitazungumza kwa haraka haraka, amesema wenzetu Tanzania Bara wamefanya utaratibu kupitia wadau pia kwa mujibu wa sheria za *ZURA* wajibu wa Wawakilishi ni sawa, na kwa mujibu wa Katiba kifungu cha 88 nikushukuru sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Nadir Abdull-latif Yussuf nakubaliana naye na maoni ya kuwa taratibu hazikufuatwa ni kweli hazikufuatwa na tutauona ukweli ukoje.

Mhe. Mohammed Said Mohammed*(Dimwa).* Nakushukuru sana kwa umakini wako jinsi shughuli zako unavyosimamia Baraza hili, namuunga mkono kwa kutumia Ilani ya Chama cha Mapinduzi Dkt. Dimwa umefanya kazi nzuri, nakushukuru sana.

Mhe. Simai Mohammed Said nikupongeze kwa dhati kabisa, katika siku uliyozungumza maneno mazito leo, ni maneno makubwa sana, maoni yako ni ya kweli, kwamba malalamiko wananchi wengi kwa jambo lake, mimi nimueleze kuwa majimbo yote wanalalamika hata Jimboni kwangu Paje wanalalamika suala hili, ukweli tuukubali tu moja itakuwa moja tu hata

ukiifanya mbili itakuwa na tumbo usiogope Waziri kukosolewa, athari za ongezeko la umeme zinagusa kila wananchi Mhe. Simai umezungumza vitu vizito sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma nikushukuru kwa aina yake wewe, wewe ndio mwenyekiti wa Kamati na nafikiri hayupo hukushirikishwa kwenye kamati hili suala na ni aibu kamati haikushirikishwa, kufika mpaka Mwenyekiti anazungumza Mhe. Naibu Spika, tunafanya nini haielekei hii, ombi lake naliunga mkono kwa Serikali kufanya wajibu wake kwa kukubali kama pahala tumeteleza tuombe radhi, si aibu, *kuteleza si kuanguka*. Hata vikombe vya chai nyumbani vinagongana, kwa hivyo Mhe. Waziri omba radhi tuendelee na mjadala huu, huko mbele tukienda Mahakamani kuzito hatuwezi kuwatesa wananchi kama hivi msiogope kukoselewa na Jaku, na mimi kiumbe vile vile.

Mhe. Hamza kaendelea tena naunga mkono maoni ya ushauri wa Serikali namna bora ya kukusanya madeni. Mheshimiwa nikitaja madeni hapa itakuwa aibu Serikali inadaiwa, nitataja baadhi ya Taasisi.

Mamlaka ya Maji inadaiwa mpaka Septemba hiyo nazungumza na hii nafikiri Mhe. Hamza alitizama tulivyofika

1)	Mamlaka ya Maji inadaiwa	Shs.16,016,312,000/=mpaka Septemba
2)	Wizara ya Afya	Shs.500,000,000/= mpaka Septemba
3)	Manispaa	Shs 881,000,000/= mpaka Septemba
4)	Idara ya Anga	Shs.883,000,000/=mpaka Septemba, Sijui Oktoba na Novemba.
5)	Sauti ya Tanzania Zanzibar	Shs. 717,000,000/=
6)	Wizara ya Kilimo	Shs.410,000,000/= mpaka Septemba hiyo
7)	Chuo cha Mafunzo	Shs.69,261,000=haijambo kidogo
8)	KMKM	Shs.127,000,000/= mpaka Septemba
9)	Afisi ya Rais Ikulu	Shs.313,000,000/= mpaka Septemba hiyo, *Hansard* zikae sawa

10)	Afisi ya Baraza la Wawakilishi	Shs. 19,000,000/= pesa ndogo sana hiyo, nalipongeza Baraza la Wawakilishi.
11)	Uwanja wa Amaan	Shs. 103,000,000/= mpaka Septemba inadaiwa.
12)	ZBC TV	Shs. 191,000,000/= mpaka Septemba
13)	Idara ya UUB	Shs. 27,000,000/= Haijambo kidogo
14)	Bandari Huru	Shs. 9,000,000/= Haijambo kidogo

Hawa viongozi wengine siwezi kutaja wa Serikali nitaona haya kidogo, lakini mpaka Marais wastaafu wamo humu, hili nitalifunika mpaka Mawaziri wastaafu siwezi kuwataja.

15)	Afisi ya Makamu wa Pili	Shs.16,000,000/= Hongereni sana,
17)	Chuo cha Utalii	Shs. 8,000,000/=
18)	Idara ya uchapaji	Shs. 39,000,000/=
19)	Mrajis Mahakama Kuu	Shs. 8,000,000/= haijambo kidogo
20)	Chuo cha Ufundi Karume	Shs. 80,000,000/=
21)	Chuo cha Afya Mbweni	Shs. 23,000,000/=
22)	Benki ya Damu	Shs.118,000,000/=
23)	Bohari Kuu ya Dawa	Shs. 97,000,000/=

Narudia tena Hansard zikae sawa, mpaka Septemba pengine wamekwenda kulipa Oktoba/Novemba sijui, lakini si rahisi hicho kitu.

24)	Wizara ya Uvuvi na Mifugo	Shs. 7,000,000/=
25)	Wizara ya Elimu	Shs.17,000,000/=

Mpaka Rais mwengine humu hii ndio hali, kweli Mhe. Hamza Hassan kazungumza maneno mazito, ndio tulipofikia hapa kuwabana wananchi wetu, kuku anataga yai moja la dhahabu ukenda kumchinja utakosa yote, kwa hoja hizi Serikali ikubali tuliyoyazungumza haya maneno ni ya kweli.

Sasa nije na Mhe. Naibu Waziri hoja yake, yeye amesema viwango vilivyolipwa ni vidogo kulingana na Tanzania Bara mimi sina tatizo na hilo, nilisema mapema nirudie mara ya pili sina tatizo, sheria tufuate kurekebisha sheria kwani kuna aibu? Hakuna aibu rekebisheni sheria tulete tena si aibu, mimi sikupi nga hapa nilisema katika hoja yangu.

Nikiwa Mwakilishi wa Wananchi jimbo la Paje, nikiwa pia nina wajibu wa nchi yangu, sina tatizo na juhudi zote za Serikali kuliwezesha Shirika la Umeme kuongeza wigo wa mapato, sina tatizo nalo.

Lakini tumeshuhudia, hapa tumekamata ng'ombe wa watu baadae tukaleta sheria, leo tunaleta sheria tena hapa hapa Baraza hili hili tunaikiuka, tunafanya nini Mhe. Naibu Waziri?

Sasa nije kwa Mhe. Waziri msomi, Mhe. Salama Aboud mimi nilikuwa namuomba tena alikuwa asichangie Mhe. Waziri, maana yake haya anajizonga mwenyewe, amesema utaratibu umefuatwa, naomba anieleze kifungu cha 36 cha Sheria ya *ZURA* kimetaka matangazo yote yatolewe na *ZURA* kwenye gazeti, yako wapi? Niletee nione, nipe ushahidi *(Makofi).*

Mhe. Waziri *ZURA* itoe mapendekezo ya maoni ya wananchi, yako wapi, tuletee tuone tusiuziane mbuzi kwenye gunia, lete ushahidi tuuone MheWaziri, huwezi kuniuzia maua juu ya muembe yanaweza yakazaa au yakapukutika yale, naomba kama kweli maoni ya wananchi yamekusanywa tuletewe tuone, kumbukumbu ziko wapi, na wakati wananchi walipitiwa kisheria tulivyotaka, lete ushahidi tuone, ukishaleta ushahidi kuna tatizo gani. Mimi sikulewa kuja kuleta matatizo haya, niko makini kusimamia hiyo Mhe. Waziri *(Kicheko/Makofi)*

Mimi naona, bado nasisitiza …

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku una dakika zako nne za kuzungumza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Bado nasisitiza kuwa wananchi hawajashirikishwa, kumbukumbu hazipo, leteni kumbukumbu tuzione humu ndani zikae sawa, kumbukumbu wananchi hamkurikodi mkaona kukoselewa na Jaku nimewaadhiri wote, mimi Jaku ni mtu mdogo sana tu mimi. Mamlaka ya kutangaza bado ni ya *ZURA,* kama *ZURA* iliyotangaza bei za mafuta karibuni mbona Mhe. Waziri hajatengeneza matengenezo yenyewe *ZURA,* haya mambo ya maajabu.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, mimi nikusifu tu na ndivyo inavyotakiwa mwizi hawezi kusema mwizi, Kiswahili hichi, ni msemo huo, nasema tena isije ikafika nikaambiwa nimesema mwizi, aa, nasema msamiati haitukatazi kuzungumza. Mwizi hawezi kusema kama mimi nimeiba. Mimi nikupongeze sana endelea tena hivi kuwatetea ndio wajibu wako unafanya kazi nzuri *(Makofi)*

Lakini Mhe. *AG* usiogope kukoselewa na Jaku, mimi ni mtu mdogo sana, naomba mapendekezo yangu yafanyiwe marekebisho Mheshimiwa kidogo tu nisisitize maoni yangu yale.

1. Kuwa Baraza hili liendelee kumtaka Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kusitisha mara moja muda wa utekelezaji wa Tangazo lake la kuongeza bei ya umeme hadi pale utaratibu sahihi wa kisheria utakapofuatwa, kwa mujibu wa Sheria ya *ZURA* na Baraza hili, kupitia kwenye Kamati yake ya kisekta kusimamia na kuona taratibu zinafuatwa mpaka mwisho.

2. Baraza hili lisimamie mamlaka yake ya kutunga Sheria na kutaka Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, isifanye majukumu ambayo Baraza hili limeyatunga kisheria kwa mamlaka nyengine. Tumepitisha hapa Sheria mimi ninayo hii hapa.

3. Zoezi la kusimamia ongezeko la umeme lianze tena upya. Si aibu kwa *ZURA* kuchukua jukumu lake kwa mujibu wa sheria au *ZURA* yenyewe Mhe. Waziri wanakumbuka wanalia pembeni.

4. Taarifa ya utekelezaji mara moja maazimio haya yawasilishwe ndani ya Baraza hili.

5. La mwisho Baraza hili liazimie Serikali kufuata sheria. *(Makofi)*

Haya ndio maazimio yangu Mhe. Naibu Spika, naomba Wajumbe muniunge mkono hoja hii, hii yetu sote, na wengi wetu humu chombo hichi ni cha wananchi, na wananchi ndio waliotutuma tuje tuwasemee matatizo yao; kwa hivyo nakuombeni sana tuunge hoja hii mkono. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Sasa kutokana na mapendekezo aliyoyatoa Mhe. Jaku, na kutokana na kuwa tayari maelezo yaliyotolewa na Mhe. Waziri wa Ardhi, lakini pamoja na maelezo yaliyotolewa na Serikali, mimi nafikiria nichukue uamuzi wa kuliuliza Baraza kama wanakubaliana na mapendekezo ya Mhe. Jaku, wanaokubaliana wanyooshe mikono.

Makatibu naomba muhesabu, Mhe. Jaku mkono mmoja tu ndio unahesabiwa kama kura, wanaokataa wanyooshe mikono, naomba uhesabu wanaokataa kwa sababu wengine watakuwa hawana.

Hoja imepigiwa kura na hoja ilikuwa kwamba Baraza likubali au likatae maoni ya Mhe. Jaku ambayo ametoa kwa kuipa Serikali; sasa waliokubaliana na maoni ya Mhe. Jaku ni 12 na waliokataa ni 27, lakini hapo hapo kuna wajumbe wengine hawakupiga kura. Sasa mimi nataka kusema nafikiri jibu tumeshalipata kwamba waliokataa hoja ya Mhe. Jaku wameshinda.

Tumeshamaliza hoja hii sasa basi. Nina tangazo moja hapa mbele yangu; ni kwamba Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari (Mhe. Ali Suleiman Ali) anawatangazia wajumbe wa Kamati wakutane katika chumba Na. 3 juu mara baada ya kuahirishwa kikao cha Baraza.

Jengine Waheshimiwa Wajumbe nataka nikukumbusheni kwamba tukitoka hapa kutakuwa na semina ya Kanuni, nawaomba sana nyote mliokuwepo hapa muhudhurie semina hii, lakini naomba nisisitize alilolisema Mhe. Spika, hususan kwa Mawaziri, kaomba sana wahudhurie semina za Kanuni kwa sababu ni wachache sana ambao wanahudhuria semina za Kanuni, ambazo ni muhimu sana pia kwa Waheshimiwa Mawaziri.

Baada ya kusema hayo sasa naahirisha kikao hadi kesho tarehe 25/11/2016 saa 3.00 asubuhi

(Saa 06.14 mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 25/11/2016 saa 3.00 asubuhi)